

# **Masomo katika umuhimu wa Tawhiidi Muhtasari wa kitabu cha Al-Usulu AL-Thalathah**

**Saleh bin Fawzan Al-Fawzan**

Kitabu hiki kinazungumzia masomo

katika umuhimu wa Tawhiid

kimezungumzia: Walaa na Balaa, na

uislam ndio dini ya nabii Ibrahim,

Niwajibu kwa Mwanadamu amuabudu

Mwenyezi Mungu peke yake, jambo

kubwa alilo amrisha Mwenyezi Mungu

waja wake ni Tawhiidi, na Nini maana

ya Tawhiidi.?

<https://islamhouse.com/2775021>

- Masomo katika umuhimu wa Tawheed. Muhtasari wa kitabu cha Al-Usulu AL-Thalathah
  - Utangulizi:
    - ILIMU
    - MWENYEZI MUNGU AKUREHEMU:
    - NILAZIMA JUU YETU KUJIFUNDISHA MAMBO MANNE.
    - MAS'ALA MANNE:
    - JAMBO LA KWANZA: ILIMU.
    - KUMJUA MWENYEZI MUNGU:
    - NA KUMJUA MTUME WAKE:

- NA KUIJUA DINI YA KIISLAM.
- KWA DALILI.
- KUIFANYIA KAZI ELIMU
- JAMBO LA PILI:  
KUIFANYIA KAZI.
- KULINGANIA KATIKA ILIMU.
- JAMBO LA TATU:  
KUILINGANIA KWAKE.
  - KUFANYA SUBRA JUU YA MAUDHI YANAYO PATIKANA NDANI YAKE.
  - JAMBO LA NNE:
  - KUFANYA SUBRA JUU YA MAUDHI YANAYO PATIKANA NDANI YAKE.

- NI LIPI JIBU LA KIAPO?
  - NA AKASEMA IMAMU BUKHARI (».a):  
MLANGO UNAO ELEZEA ILIMU KABLA YA KAULI NA MATENDO.
  - RISALA YA TATU MAMBO MATATU NI LAZIMA MUISLAM AJIFUNDISHE NA AYAFANYIE KAZI.
  - NI LAZIMA JUU YA KILA MUISLAM WAKIUME NA WAKIKE,
  - YEYOTE ATAKAE MTII ATAINGIA PEPONI, NA YEYOTE ATAKAE

## MUASI ATAINGIA MOTONI.

- MAS'ALA YA PILI:
  - WALAA NA BARAA.
  - UJUMBE WA TATU  
UISLAM NDIO DINI YA  
NABII IBRAHIM.
  - NA MAANA YA QAULI YA  
MWENYEZIMUNGU {ILI  
WANIABUDU}.
  - JAMBO KUBWA ALILO  
AMRISHA MWENYEZI  
MUNGU WAJA WAKE NI  
TAUHIIDI.
    - NINI MAANA YA  
TAUHIDI?
  - Utangulizi:
  - Jambo kubwa alilo liataza  
Mwenyezi Mungu ni Shirki.

- Maana ya Shirki.
- Dalili inayo onyesha kuwa Tawhiidi ni jambo kubwa alilo amrisha Mwenyezi Mungu.
- Ujumbe wa Nne Misingi mitatu ambayo ni lazima kuifahamu.
- Kwanini ameihusisha misingi hii mitatu?.

## Masomo katika umuhimu wa Tawheed. Muhtasari wa kitabu cha Al-Usulu AL-Thalathah

### Utangulizi:

Kaanza kwa kusema Bismi llahi Rahmani Rrahim; Kwajina la Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma mwenye kurehemu.

Ameanza Mwenyezi Mungu  
Amrehemu risala hii kwa jina la  
Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma  
mwenye kurehemu, kwa kufuata  
kitabu cha Mwenyezi Mungu mshindi  
na mtukufu, kwa sababu macho yako  
yakiangalia ndani ya msahafu na kabla  
ya kila sura kuna (**Bismi llahi  
Rrahmani Rrahim**).

Kuanzia neno hili katika risala na  
katika vitabu nikufuata kitabu cha  
Mwenyezi Mungu mshindi na  
mtukufu, vilevile nabii Muhammad  
(s.a.w) Alikua -ana mwambia  
muandishi- a'ndike mwanzo wa kila  
barua wakati anapo watumia viongozi  
na maraisi na waliyoko mbali ana

walingania katika Uislamu, **anaanza kuandika:**

Kwajina la Mwenyezi Mungu  
Mwingi wa rehma mwenye kurehemu.

Na alikua Mtume (**s.a.w**) anaanza mazungumzo yake na maneno yake kwa: Bismi llahi Rrahmani Rrahim, yaonyesha kuanza kwa Bismi llahi Rrahmani Rrahim ni sunna ya Mtume (**s.a.w**), vilevile Nabii Sulaiman (**s.a.w**) alipo muandikia Malkia -Mfalme wa saba' Yemen- **ameanza kuandika kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehma mwenye kuruhemu:** (Malkia akasema: Enyi wahishimiwa! Hakika nimeletewa barua tukufu\* Imetoka kwa Sulaiman nayo ni.

Kwajina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehma Mwenye kurehemu\* Msinifanyie jeuri, na fikeni kwangu nanyi mmekwisha kuwa wenyewe kusalimu amri).

(An-Naml: 29-31).

Inatakiwakuanza na jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehma Mwenye kurehemu, katika kila jambo lenye umuhimu, na katika kila kitabu chenye umuhimu na thamani, na katika kila risala.

Kwa sababu hii wale ambao hawaanziki kwenye vitabu vyao na risala zao kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehma Mwenye kurehemu, hao wameacha sunna ya Mtume na kuto

kufuata kitabu cha Mwenyezi Mungu Mshindi na mtukufu, huenda kwa sababu hiyo vitabu vyao na risala zao hazina baraka na ndani yake hakuna faida; kwa sababu ikiwa hakuna jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehma Mwenye kurehemu huondolewa faida.

Risala ya kwanza Maswala manne ambayo yameambatana na Surati Al-Asr,

## **ILIMU**

Tambua Mwenyezi Mungu akurehemu.

Hili ni neno linalo ashiria umuhimu wa mada, **anapo sema:** Tambua: lina maana ya kwamba atakacho kwambia nimuhimu sana.

## **MWENYEZI MUNGU** **AKUREHEMU:**

Hii ni dua kwa mtafutaji wa Ilimu, anawaombea watafutaji wa elimu Mwenyezi Mungu awarehemu, na awape rehma zake, maneno haya ndani yake kuna upole kutoka kwa mwalimu kwenda kwa mwanafunzi, na kwamba yeye anaanza kwa maneno mazuri na dua njema, mpaka awaathiri kwa maneno hayo na wamuelekee mwalimu wao.

Lakini mwalimu akianza maneno kwa ukali na maneno yasio faa jambo hili lina wakimbiza -wanafunzi-, wajibu wa mwalimu na wale wanao lingania katika njia ya Mwenyezi Mungu, na

nijuu ya yule anae amrisha mema na  
kukataza mabaya kuwa mpole kwa  
yule anae ongea nae, kwa kumuombea  
dua na kumsifu kwa maneno laini,  
kwani hili lapelekea kukubali.

Lakini mtu mwenye kiburi mjeuri,  
yeye ana maneno maalumu, **Amesema  
Mwenyezi Mungu Mtukufu:**

(Wala msijadiliane na watu wa kitabu  
ila kwa njia iliyio nzuri kabisa, isipo  
kuwa wale walio dhulumu miongan  
mwao. **Na semeni:** Tumeyaamini  
yaliyorremshwa kwetu na  
yaliyorremshwa kwenu. Na Mungu  
wetu na Mungu wenu ni Mmoja. Na  
sisi ni wenyewe kusilimu kwake).

(Al-Ankabut: 46).

Wake walio dhulumu nafsi zao  
miongoni mwa walio pewa kitabu,  
wakafanya ujeuri na kiburi, hao  
hawalinganiwi kwa upole, wao  
hulinganiwa kwa ukali. Amesema  
**Mwenyezi Mungu Mtukufu.**

(Ewe Nabii! Pambana na makafiri na  
wanaafiki, na wakazanie. Na makaazi  
yao ni Jahannamu, na huo ndio  
mwisho mbaya).

(At-Tawba: 73).

Wanaafiki hawajadiliwi kwa silaha,  
lakini hujadiliwa kwa hoja na maneno  
makali, nakuwatahadharisha watu  
wasiwe karibu nao, na Amesema  
**Mwenyezi Mungu Mtukufu:** (Na

uwaambie maneno ya kuathiri na kuingia katika nafsi zao).

(An-Nisaa: 63).

Hao wana maneno yao maalumu; kwa sababu wao ni wapingaji wenye viburi, wala

hawataki haki bali wanataka kuwapoteza watu, hao huambiwa kwa wanayo stahiki.

**NILAZIMA JUU YETU**  
**KUJIFUNDISHA MAMBO**  
**MANNE.**

Jambo hili sio hiyari, wala sio lenye kupendeza -ukitaka unafanya hukutaka unaacha- isipo kua ni lazima hasa.

Tutapo acha kujifundisha mambo haya kwa hakika tuna pata madhambi, kwa sababu jambo hili ni lazima, **hakusema:** ni hiyari kwetu au yapendeza kwetu, **lakini kasema:** ni lazima kwetu, **na jambo lazima maana yake:** mwenye kuliacha hupata dhambi, na kwa sababu elimu haipatikani isipo kuwa kwa kujifundisha, na kujifundisha kuna hitaji umuhimu na juhudhi na muda, na kuna hitaji ufahamu na kuhudhurisha moyo, huku ndiko kujifundisha.

Mwenyezi Mungu Anasema katika Suratul Asr: kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehma mwenye kurehemu (**Naapa kwa Zama!\*** Hakika binaadamu bila ya shaka yumo katika

khasara\* Isipokuwa wale walio amini, na wakatenda mema, na wakausiana kwa haki, na wakausiana kusubiri).

(Al-Asr: 1-3).

### **MAS'ALA MANNE:**

yaani upekuzi, yameitwa mas'ala; kwa kuwa mambo hayo nilazima kuulizwa na kutiliwa umuhimu.

### **JAMBO LA KWANZA: ILIMU.**

Ilimu: makusudio ya ilimu hapa ni elimu ya kisheria; kwa sababu ndio ambayo ni lazima kujifundisha, na mas'ala haya ni lazima kujifundisha kwa kila Muislam, mwanamume au mwanamke, alie huru au mtumwa, tajiri au maskini, mfalme au raiya. Kila

Muislam ni lazima kwake kujifundisha mas'ala haya manne.

Na hili ndio linaloitwa na wanachuoni Ulazima waki pekee, ndio ambao ni lazima kwa kila mmoja katika Waislam, swala tano kwa wanamume na wanawake, na swala ya jamaa misikitini kwa wanamume. Jambo hili ni lazima kwa kila Muislam kujifundisha, **kwa sababu hiyo alisema:** ni lazima juu yetu, **na hakusema:** ni lazima kwa baadhi yetu, **ila kasema:** ni lazima juu yetu, yaani sisi Waislam, **hii nikatika elimu ambayo ni lazima kwa kila mtu;** **kwa sababu elimu zipo namna mbili:** Jambo la kwanza ambayo ni lazima kwa kila mtu kujifundisha, hakuna udhuru kwa

asiye jifundisha, nayo niile ambayo  
haisimami dini bila yenyewe, **mfano  
nguzo za Uislamtano ambazo ni:**

A.Shahada mbili,

B.kusimamisha Swala,

C.kutoa Zaka,

D.kufunga Mwezi mtukufu wa  
Ramadhani,

E. Kuhiji nyumba ya Mwenyezi  
Mungu,

Haifai kwa Muislam kuto juu mambo  
haya ni lazima kujifundisha.

Kwa sababu kujifundisha maana ya  
Shahada mbili ndiko kujifundisha  
Tauhidi, anajifundisha Muislam

tauhidi ili aifanyie kazi, na ajifundishe yanayo kwenda kinyume na tauhidi ili ajiepushe nayo, haya ndio mafungamano ya Shahada mbili, vilevile ajifundishe nguzo za swala na sharti zake, na ylio yalazima ndani ya swala, na sunna za swala.

Vilevile ajifundishe hukumu za zaka, na ajifundishe hukumu za funga, na ajifundishe hukumu za hija, anapotaka kuhiji ni lazima ajifundishe hukumu za hija na hukumu za umra, ili atekeleze ibada hizi katika njia ilio amrishwa.

Na kipengele hiki hakuna udhuru kwa yejote kuto kijua, nacho kinaitwa ulazima wa kila Muislam.

Sehemu ya pili katika vigawanyo vya elimu: nayo ni tofauti na elimu ya kisheria ambayo umma unaihitaji kwa ujumla wake, nasio kila mtu huihitaji, mfano hukumu za kuuza na kununua na hukumu za muamala, na hukumu za kutoa wakfu, na mirathi na usia, na hukumu za kuo, na hukumu za makosa ya jinai, mambo haya nilazima kwa umma; lakini sio lazima kwa kila mtu kujifundisha, **isipokuwa watapo jifundisha wenye kutosheleza na malengo yakatimia miongoni mwa wanachuoni yatosha; jambo hili linaitwa:** faradhi kifaya, wakifanya baadhi ya watu madhambi huondoka kwa wengine, na watapo liacha wote basi hupata dhambi wote.

Ilimu ya lazima ndio ambayo ataulizwa mja siku ya kiyama, **kwa nini hukujifundisha?** Kwa nini hukuuliza? Ilimu ambayo ataisema **pindi atapo wekwa ndani ya kaburi:** Mola wangu ni Mwenyezi Mungu, na Uislam ndio dini yangu, na nabii wangu ni Muhammad (**s.a.w**) jambo hili laokoa, **ataambiwa:** umejifundisha wapi? Atasema: nimesoma kitabu cha Mwenyezi Mungu na nikajifundisha.

Ama Yule alie jitenga mbali na elimu hiyo kwa hakika atapo ulizwa katika kaburi lake atasema: hahahaha sijuwi niliwasikia watu wakisema jambo Fulani nami nikalisema.

Mtu kama huyu atawashiwa moto  
ndani ya kaburi lake -Allah atunusuru-  
na kaburi litambana hadi mbavu zake  
hupishana, na kaburi lake huwa ni  
shimo miongoni mwa mashimo ya  
moto wa Jahannam; kwa sababu yeye  
hakutaka kujifundisha wala kusoma,  
**ataambiwa:**

**(Hukutaka kujifundisha wala kusoma).**

Kapokea hadithi hii Imam Bukhari  
kwa ufupi kwa hadithi ya Anas (1338)  
na kaipokea pia Imam Muslim kwa  
ufupi hadithi ya Anas (».a) (2870).

Na kaipokea Abuudaud kwa hadithi ya  
Bara' bin A'zib (».a) kwa urefu (4752).

Yeye hakujifundisha, wala  
hakuwafuata wanachuoni, bali yeye  
kapoteza uhai wake, huyu ndio ambae  
atakua sehemu mbaya -Allah  
atunusuru.

**ILIMU:** Hii ndio ilimu ya kisheria,  
kinacho takiwa kwa ujumla wetu na  
mmoja mmoja nako nikumjua  
Mwenyezi Mungu kwa Majina yake na  
Sifa zake, na kujua haki zake juu yetu,  
nayo ni Kumuabudu yeye peke yake  
hana mshirika katika u'ngu wake,  
jambo la kwanza kulitambua  
mwanadamu ni kumjua Mola wake  
Mtukufu, na namna ya kumuabudu.

NA KUMJUA MWENYEZI  
MUNGU, NA KUMJUA MTUME  
WAKE.

## **KUMJUA MWENYEZI MUNGU:**

Vipi mja atamjua Mola wake? Atamjua kwa alama zake na viumbe wake, **miongoni mwa alama za kumjua kwake:** usiku na mchana, **na katika viumbe vyake:** jua na mwezi, kama tunavyo bainisha hapa kwa matakwa ya Allah.

Hujulikana Mwenyezi Mungu kwa alama zake za kidunia na Aya zake za qur-ani. Anapo soma qur-ani, humtambua Mwenyezi Mungu Mtukufu kwamba ye ye ndio ambae kaumba mbingu na ardhi, naye

Mwenyezi Mungu ndie ambae kavifanya kuwa vyepesi vilivyoko mbinguni na ardhini, naye Mwenyezi Mungu ndie ambae Ana huisha na kufisha, naye nimuweza juu ya kila kitu, naye ni Mwingi wa rehma mwenye kurehemu, Qur-ani ina mtambulisha Mwenyezi Mungu Mtukufu, naye Mwenyezi Mungu ndie ambae Ametune'mesha ne'ma zote, naye Mwenyezi Mungu ndie Alie tuumba na kuturuzuku, utapo soma qur-ani utamjua Mola wako Mshindi na Mtukufu kwa Majina yake na Sifa zake na vitendo vyake.

Na utakapo angalia katika hii dunia utamtambua Mola wako Mtukufu kama ye ye ndie alie umba, na

akafanya wepesi katika huu  
ulimwengu na akaupitisha kwa hikma  
yake na kwa Ujuzi wake, Hii ndio  
Elimu ya kumjua Mwenyezi Mungu  
Mtukufu.

### **NA KUMJUA MTUME WAKE:**

Yeye ni Muhammad (**s.a.w**) kwa  
sababu yeye ni Mwenye kufikisha  
niaba ya Mwenyezi Mungu Mtukufu,  
na yeye niwakati baina yetu na  
Mwenyezi Mungu Mtukufu katika  
kufikisha ujumbe, hapana budi  
kumjua, unafahamu yeye ni nani?  
Unafahamu ukoo wake?

na ujuwe mji wake, na ujuwe aliyo  
kuja nayo (**s.a.w**) unafahamu namana  
Wahyi ulivyo anza kushuka? Na

namna alivyo simama katika kulingania katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu katika mji wa Makkah na Madina, unajua hestoria ya mjumbe wa Mwenyezi Mungu (**s.a.w**) japo kwa ufupi?

Mtume (**s.a.w**) yeye ni Muhammad bin Abdullah bin Abdul muttwalib bin Hashim bin Abdi manafi mpaka mwisha wa nasabu ya mtume mtukufu ambayo inaishia kwa NaBii Ibrahim (**s.a.w**), na unajua namna alivyo ishi kabla ya utume, na namna alivyo jiwa na wah'yi kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na nini alichoh fanya (**s.a.w**) baada ya kupewa utume, utayajua yote hayo kwa kusoma hestoria yake (**s.a.w**). na haifai kwa

Muislam kutomjua mtume (**s.a.w**) vipi unamfuata mtu hali yakua humjuwi?!  
Haiingii akilini.

## **NA KUIJUA DINI YA KIISLAM.**

Kuijua dini ya kiislam: ambayo ndio dini ya huyu Mtume (**s.a.w**) bali ndio dini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ambae kawaamrisha kwa dini hiyo waja wake, naye ndio ambae amekuamrisha kuifuata, na wewe watakiwa kuifuata, hapana budi kuijua hii dini, na Uislam ndio dini ya Mitume wete. Mitume wete dini yao Uislam kwa maana ya ujumla, ye yote alie mfuta Mtume miongoni mwa Mitume huyo ni Muislam mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu mwenye

kumfuata yeye, mwenye kumpwekesha yeye.

Huu ndio Uislam kwa maana ya ujumla, hakika ni dini ya Mitume wote, Uislam nao ni kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu kwa tauhidi, na kumfuata yeye kwa kutii, na kujiepusha na ushirikina na watu wake.

Ama Uislam kwa maana yake halisi niule ambao amemtuma nao Mwenyezi Mungu Mtume wake Muhammad (s.a.w) kwa sababu baada ya kutumwa Mtume (s.a.w) hakuna dini isipokuwa dini yake (s.a.w), na Uislam umehusishwa katika kumfuata yeye (s.a.w) haiwezekani Yahudi akasema: Mimi ni Muislam, au Naswara aseme:

Mimi Muislam baada ya kutumwa Mtume (s.a.w) haliyakua hamfuati, Uislam baada ya kutumwa Mtume (s.a.w) ni kumfuata, Amesema **Mwenyezi Mungu Mtukufu:** (Sema: Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni mimi, Mwenyezi Mungu atakupendeni.

(Al-**Imran:** 31).

Huu ndio Uislam kwa maana ya ujumla na kwa maana yake halisi.

## **KWA DALILI.**

Kwa dalili: sio kwa kuiga lakini kwa dalili katika Qur-ani na Sunna, hii ndio elimu.

Amesema Ibnul-QaYyim katika kitabu chake Al-kafiyatu shafiya:

Ilimu kasema

Mwenyezi Mungu kasema Mtume wake kasema Swahaba hao ndiyo wajuzi Siyo elimu inayo sababisha tofauti za kijinga kati ya Mtume na maoni ya Fulani, hii ndio elimu.

Elimu ni ile elimu ya kitabu(Quraan) na sunna, na kuhusu maneno ya wanachuoni yenyewe husherehesha na kuweka wazi zaidi maneno ya Mwenyezi Mungu na maneno ya Mtume wake (s.a.w)

Na kwa hakika ndani ya maneno hayo au baadhi yake huwa kuna makosa.

## **KUIFANYIA KAZI ELIMU**

### **JAMBO LA PILI: KUIFANYIA KAZI.**

Kuifanyia kazi, **maana yake**: kwa elimu kwa sababu mwanadamu anafundisha na ana jifundisha hapana budi kuifanyia kazi elimu yake, elimu bila matendo itakua ni hatari kwa mwenye nayo, haiwi elimu yenye manufaa ila kwa matendo, ama Yule alie jifundisha na hakuifanyia kazi elimu yake huyo kakasirikiwa; kwa sababu yeye kaijuwa haki na akaiacha kwa elimu.

Mtunzi anasema: **(Na Mwanachuoni hakuifanyia kazi elimu yake)**

Ataadhibiwa kabla ya wenyе kuabudia Masanamu).

Na jambo hili limetajwa kwenye hadithi tukufu: (Mtu wa mwanzo kuingizwa katika moto siku ya kiyama, Mwanachuoni ambae hakuifanyia kazi elimu yake).

Kapokea hadithi hii Imam Tirmidhi (2382).

nayo ni hadithi ndefu ndani yake: (Hao wenyе sifa tatu ndio wa mwanzo kabisa kuingizwa katika moto siku ya kiyama), hadithi ya Abaa huraira (».a).

Elimu imeambatanishwa na vitendo, na vitendo ndio matunda ya elimu, elimu bila vitendo ni kama mtu bila

matunda, hauna faida ndani yake, na elimu imeletwa ili ifanyiwe kazi.

Kama yalivyo matendo yasio kua na elimu inakua ni msiba na upotevu kwa mtendaji.

Ikiwa mwanadamu anafanya matendo bila elimu kwa hakika matendo yake yana kuwa ni msiba na tabu kwa mtendaji, Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (**s.a.w**):

(Yeyote atakae fanya Amali hakuna Amri yetu yatakuwa ni yenye kurejeshwa).

Kapokea hadithi hii Imam Bukhari kabla ya hadithi (**7350**), na Muslim (18/1718), hadithi ya Bibi Aisha (**✉.a**).

na kapokea Bukhari (2697) na Muslim (17/1718) kutoka kwa Bibi Aisha (رض). Amesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ): (Yeyote atakae zua katika dini yetu hii jambo lisilo kuwemo atarejeshewa).

Na kwa sababu hii tuna soma katika suratul Fatiha katika kila raka:  
(Tuongoze njia iliyo nyooka\* Njia ya wale ambao uliyo waneemesha, siyo ya wale waliyo kasirikiwa na wala waliyo potea).

(Al-Fatiha: 6-7).

Akataja Mwenyezi Mungu wale ambao wanafanya bila elimu walio potea, na wale ambao wanafahamu na hawayafanyii kazi wamekasirikiwa,

tuzindukane na jambo hili kwa sababu ni muhimu sana.

## **KULINGANIA KATIKA ILIMU.**

### **JAMBO LA TATU:** **KUILINGANIA KWAKE.**

Kuilingania katika njia ya Mwenyezi Mungu: maana yake: haitoshi kujifundisha mwanadamu na akafanya pekeyake, wala asilinganii katika njia ya Mwenyezi Mungu Mshindi na Mtukufu, hapana budi awalinganie wengine, ili ainufaishe nafsi yake na nafsi za wengine, na kwa sababu elimu hii ni amana, sio milki yako ukawa unailimbikiza tu na una wanyima watu, na watu wana shida nayo, ilio wajibu kwako kufikisha na kubainisha na

kuwalingania watu katika kheri,  
hapana budi kuifikisha na kuibainisha  
kwa  
watu.

Am

**esema Mwenyezi Mungu Mtukufu:**  
**(Na pindi Mwenyezi Mungu alipo**  
**funga ahadi na walio pewa Kitabu**  
**kuwa: Lazima mtawabainishia watu,**  
**wala hamtokificha).** (Al-'Imran: 187).  
Ahadi hii kaichukua Mwenyezi Mungu  
kwa Wanachuoni wawabainishie watu  
yale walio fundishwa na Mwenyezi  
Mungu ili waeneze kheri, na  
wawatowe watu katika gize kuwaweka  
katika nuru, Hii ndio kazi ya Mitume  
**(s.a.w)** na wafuasi wao, **Amesema**  
**Mwenyezi Mungu Mtukufu:** (Sema:  
Hii ndiyo njia yangu ninalingania kwa

Mwenyezi Mungu kwa ilimu mimi na wanao nifuata.

Na ametakasika Mwenyezi Mungu!  
Wala mimi si katika washirikina).  
(Yusuf: 108).

Hii ndiyo njia ya Mtume (s.a.w) na nhia ya wafuasi wake, ilimu na matendo na kulingania kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, yejote asie lingania haliyakuwa anao uwezo wa kulingania na ilimu anayo akaificha, kwa hakika atafungwa kamba za moto mdomoni mwake siku ya kiyama kama ilivyo katika hadithi. Kaipokea Abuu daudi (3658), na Tirmidhi (2649), na Ibnu Maja (261) na (266) hadithi ya Abaa huraira (s.a) Amesema: Amesema

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w): (Yeyote atakae ulizwa katika mambo ya ilimu akaficha, atafungwa kamba na Mwenyezi Mungu za moto mdomoni mwake siku ya kiyama). Na Ibnu Maja (265) kwa hadithi ya Abii Saidi l-khudri (✉.a) Amesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w): (Yeyote atakae ficha Elimu katiaka Elimu anazo wanufaisha Mwenyezi Mungu watu, mambo ya dini, Allah atamfunga siku ya kiyama kamba za moto mdomoni mwake).

**KUFANYA SUBRA JUU YA  
MAUDHI YANAYO PATIKANA  
NDANI YAKE.**

**JAMBO LA NNE:**

## **KUFANYA SUBRA JUU YA MAUDHI YANAYO PATIKANA NDANI YAKE.**

Subra juu ya maudhi yanayo patikana  
ndani yake:

kama inavyo julikana yeote ane  
walingalia watu aka waamrisha mema  
na aka kataza mabaya, kwa hakika  
atafikwa na maudhi kwa watu waovu;  
kwa sababu watu wengu hawapendi  
kheri, bali hupenda matamaniyo na  
haramu na matakwa ya nafsi yaliyo  
mabaya, anapokuja mwenye  
kuwalingania kwa Mwenyezi Mungu,  
na kukemea matamanio yao, hapana  
budi.

Miongoni mwao kufanya vibaya ima  
kwa maneno au kauli,

Ni lazima juu ya mwenye kulingania  
katika njia ya Mwenyezi Mungu na  
kutaka radhi za Mwenyezi Mungu  
asubiri maudhi, na aendelee katika  
kulingania, na kiigizo chake ni Mitume  
(s.a.w) na mbora wao na wa mwisho  
wao Muhammad (s.a.w).

Yamemfika mangapi kutoka kwa  
watu? Na maudhi mangapia kayapata  
kwa maneno na vitendo? Walisema:  
mchawi, muongo, **wakasema:**  
mwandawazimu. Wakasema dhidi  
yake maneno ambayo ameyataja  
Mwenyezi Mungu Mtukufu ndani  
ya Qur-ani, wakamfanyia maudhi,

kapigwa mawe mpaka miguu yake ikatoa damu (**s.a.w**) wakati alipo walingania katika njia ya Mwenyezi Mungu, kawekewa utumbo wa ngamia juu ya mgongo wake akiwa ana sujudu mbele ya Alkaaba, kaahidiwa kuuliwa katishwa katika vita vya Uhudi ali dhuriwa yeye na maswahaba zake (**s.a.w**),

kavunjwa memo yake manne ya mbele, kapasuliwa kichwani mwake (**s.a.w**) kasukumwa ndani ya shimo, haliyakuwa ni nabii wa Mwenyezi Mungu, madhara yote haya kayapata katika kulingania kwaajili ya Mwenyezi Mungu, lakini yeye kasubiri kavumilia haliyakua ndio mbora wa viumbe wote (**s.a.w**), hapana budi kwa

Yule anae fanya kazi ya kulingania kufikwa na maudhi kiasi cha imani yake na dawa wake; pamoja na yote hayo yatakiwa asubiri, akiwa yupo katika haki, asubiri avumilie, yupo katika njia ya Mwenyezi Mungu na maudhi yanayo mfika yatakuwa katika mizani yake mema mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Mambo haya ma nne nilazima tujifundishe kwa urefu.

Kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: (**Naapa kwa Zama!**).

(Al-Asr1).

Ameapa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa zama na wakati nao ni kiumbe, na

Mwenyezi Mungu Mtukufu anaapa kwa anacho kitaka miongoni mwa viumbe, na kiumbe haapi isipokuwa kwa jina la Mwenyezi Mungu, Na Mwenyezi Mungu haapi isipokuwa kwa kitu chenye umuhimu, na ndani yake kuna alama miongoni mwa alama zake, Utakasifu niwake na ametukuka, ndani ya zama kuna mazingatio na umuhimu, na kwa sababu hiyo Ameapa Mwenyezi Mungu kwa muda wa Laasiri, na kwa usiku unapo funika na akaapa kwa mchana. Ama kiumbe haifai kuapa isipokua kwa jina la Mwenyezi Mungu, na haifai kwetu kuapa kwa asie kua Mwenyezi Mungu, Amesema Mtume (s.a.w): (Yeyote atakae apa kwa asiye kua Mwenyezi Mungu kwa hakika amekufuru au

ameshirikisha). Kapokea hadithi hii Imam Abuu daudi (3251), na Tirmidhi (1535) kwa hadithi ya Ibni Omar (✉.a).

Na Akasema: (Yeyote anae taka kuapa Aape kwa jina la Mwenyezi Mungu au akae kimya).

Kapokea hadithi hii Imam Bukhari (6108), na Muslim (1646) kwa hadithi ya Ibni Omar (✉.a).

## **NI LIPI JIBU LA KIAPO?**

Ni kauli yake: (Hakika binaadamu bila ya shaka yumo katika hasara).

(Al-Asr: 2).

Mwanaadamu Binaadamu woote hakuvuliwa hata mmoja siyo wafalme wala maraisi, wala matajiri, wala

Mafakiri, wala walio huru, wala watumwa, wala wanamume wala wanawake, kila binaadamu yupo katika Hasara, **maana yake:** katika hasara na maangamio ikiwa wataupoteza huu muda ulio wa thamani, wakautumia katika kumuasi Mwenyezi Mungu, na katika yanayo wadhuru.

Wanaadamu weete wamo ndani ya hasara na maangamio isipokuwa atakae sifika na sifa nne nazo: Ilimu, na Matendo, na kulingania katika njia

ya Mwenyezi Mungu, na kufanya  
subra juu ya maudhi.

Yeyote atakae sifika na sifa hizi nne  
ameokoka katika hii hasara. Wala  
haiwezekani kumuamini Mwenyezi  
Mungu isipokuwa kwa Ilimu, Ambayo  
ndio kumjuwa Mwenyezi Mungu.

(Na wakatenda mema). (Al-Asr: 3).

Maana yake: wamefanya matendo  
yalio mazuri katika mambo ya lazima  
na yasio yalazima, wakatumia muda  
wao kwa matendo mema  
  
kwa yale yanayo wanufaisha katika  
dini yao na dunia yao.

Hata matendo ya kidunia ndani yake  
kuna ujira ikiwa utakusudia katika

hayo matendo kuwa ni sababu ya kufanya twaa, itakuwaje matendo kwaajili ya akhera, lamsingi jitahidi usipoteze muda utumie katika mambo yanayo kunufaisha na yanayo kufiidisha.

(Na wakausiana kwa haki). (**Al-Asr: 3**).

Wameamrisha mema, na Wamekataza mabaya, na Wakalingania katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, Na Wakafundisha Ilimu yenyе manufaa, na Wakazagaza Ilimu na kheri kwa watu.

Wakawa walinganiaji katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

(Na wakausiana kusubiri). (**Al-Asr: 3**).

Walifanya subra kwa yale walio  
yapata,

Na Subra katiak lugha ya kiarabu:  
kuziwia, **lakini makusudio hapa:**  
kuiziwia nafsi katika kumcha  
Mwenyezi Mungu.

Nazo zipo aina tatu:

1. Kufanya subra katika kumtii  
Mwenyezi Mungu.

2. Kufanya subra kwa yale aliyo kataza  
Mwenyezi Mungu.

3. Kufanya subra juu ya makadara ya  
Mwenyezi Mungu.

1. Subra katika kumtii Mwenyezi  
Mungu, kwa sababu nafsi inapenda

uvivu na inapenda raha, hapana budi kuizoweza binaadam nafsi juu ya kutii na kusali na kufunga na kupigana jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu japokuwa mambo haya nafsi haiyapendi, anaiziwiya katika utiifi wa Mwenyezi Mungu.

## 2. Kufanya subra kwa yale aliyo kataza Mwenyezi Mungu.

Nafsi inataka mambo ya haramu, na mambo ya matamanio, inaelekea huko na kuvutiwa sana, hapana budi aifunge na kuiziweya katika mambo ya haramu, jambo hili lahitaji subra, na siyo jambo rahisi kuizuiya nafsi katika mambo ya matamanio ya haramu, ambae hana subra kwa hakika nafsi

yake itamshinda na itamvuta kwenye haramu.

3.Kufanya subra juu ya makadara ya Mwenyezi Mungu yenyeye kuu miza.

Matatizo yanayo mpata mwanaadamu kwa kufiliwa na mtu wake wa karibu, au kupoteza mali, au maradhi yanayo mpata mwanaadamu, hapana budi afanye subra juu ya hukumu na makadara ya Mwenyezi Mungu, asikate tamaa wala kuchukia, bali auziwiye ulimi na kuto omboleza na kutokata tamaa, na aiziwiye nafsi kutokata tamaa, na aziwiye viungo na kuto jipiga makofi na kuchana nguo kwa hasira, Hii ndiyo subira wakati wa matatizo.

Kuhusu maasi asifanyi subra juu yake bali atubiyе kwa Mwenyezi Mungu na ayakimbiye; lakini wakati wa mitihani ambayo hukuingia ndani yake, bali nikutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu amekukadiria juu yako na kukupa mtihani au adhabu kwako kutokana na madhambi uliyo yafanya, kama alivyo sema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

(Na misiba inayo kupateni ni kwa sababu ya vitendo vya mikono yenu. Naye anasamehe mengi). (Ash-Shura: 30).

Utapofika msiba kwa Muislam katika nafsi yake au mali zake au watoto zake au ndugu wa karibu au yejote kati ya

ndugu zake Waislam ni juu lako  
kufanya subra na kutegemea malipo  
kwa Mwenyezi Mungu.

Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

(Wale ambao ukiwasibu msiba  
husema: Hakika sisi ni wa Mwenyezi  
Mungu, na kwake Yeye hakika  
tutarejea \* Hao juu yao zitakuwa  
Baraka zitokazo kwa Mola wao Mlezi  
na rehema. Nao ndio wenye  
kuongoka).

(Al-Baqara: 156-157).

Hii ndio subra, na mfano wake  
kufanya subra juu ya maudhi unayo  
yapata katika kulingania neno la  
Mwenyezi Mungu Mtukufu hayo

nikatika matatizo, nilazima ufanye subra kwa hayo unayo yapata katika njia ya kheri, **Nawala usiachi kufanya kheri; kwa sababu baadhi ya watu wanataka kufanya kheri lakini akikutana na jambo linalo chukiza anasema:** sio lazima juu yangu kuiweka nafsi yangu kwenye mambo kama haya, kisha anaacha kufundisha ikiwa ni mwalimu, anaacha kulingania katika njia ya Mwenyezi Mungu, anaacha kuongea ikiwa ni khatwibu wa muskiti, anaacha kusalisha muskitini, anaacha kuamrisha mema na kukataza mabaya, Huyu hakusubiri kwa aliyo yapata mionganini mwa maudhi.

Amesema Imam Shaafy (✉.a):

"Laiti Mwenyezi Mungu asinge teremsha dalili kwa waja wake ila surahii ingeliwatosha".

Kwa hakika kanukuu Imam Shafy: yeeye ni Muhammad ibni Idrisa Ashaafy nasabu kwa babu yake wa nne jinalake shafy, nae ni mkuraishi, katika familia ya mutw-labi, kafariki mwaka (204) h.j.. naye ni mmoja kati ya Maimamu wa nne, na akasema maneno haya kwa sababu Mwenyezi Mungu kabainisha kwanye sura hii sababu za kupotea na sababu za kuongoka

Kuhusu sababu za kuongoka: Asifike mwanaadamu na hizi sifa nne: Ilimu, na Matendo, na Kulingania, nakufanya

subra juu ya maudhi yanayo tokea katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, ikasimama hoja kutoka mwa Mwenyezi Mungu juu ya waja wake kwa sura hii, **Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu ana waambia:** Hakika mimi Allah nime kubainishieni sababu za kuokoka katika sura hii fupi sana.

Na Qur-ani yate pamoja na Sunna vimefafanuwa zaidi mambo haya manne, lakini sura hii imebainisha sababu za kuongoka kwa ujumla, ikasimama hoja kwa viumbe, na zikabaki dalili ndani ya qur-ani na sunna ziki fafanuwa zaidi na kuweka wazi mambo haya manne, na wala sio makusudio ya Imam Shafy kwamba sura hii yawatosha watu, kama

asingliteremsha Mwenyezi Mungu sura tofauti na hii, lakini hoja imesimama juu yao; kwa sababu Mwenyezi Mungu kisha bainisha ndani yake sababu za kuokoka na sababu za uongofu, asitokei ye yote siku ya kiyama akasema:

Mimi sijuwi sababu za uongofu wala sijuwi sababu za kupotea naye akisoma sura hii fupi sana.

**NA AKASEMA IMAMU**  
**BUKHARI (ص.ا): MLANGO UNAO**  
**ELEZEA ILIMU KABLA YA**  
**KAULI NA MATENDO.**

Na dalili: (Basi jua ya kwamba hakuna Mungu anayefaa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, na omnia)

maghufira kwa dhambi zako na za  
Waumini wanaume na Waumini  
wanawake). (Muhammad: 19).

Akaanza Ilimu kabla ya kauli na  
matendo.

Bukhari: yeye ni Muhammad bin  
Ismail bin Imrahim Al-Bukhary,  
kanasibishwa na Bukhara mji uliyoko  
Mashariki, ni Imam wa Hadithi bingwa  
wa kuhifadhi (ص.ا), mtunzi wa  
(Swahili) kitabu ambacho kina usahihi  
baada ya kitabu cha Mwenyezi Mungu.

Ilimu kabla ya kauli na matendo; kwa  
sababu matendo hayanufaishi  
isipokuwa yakijengewa juu ya ilimu,  
lakini matendo yaliyo jengeka juu  
kutenda.

Na dalili: kuhusu kichwa cha habari  
kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:  
(Basi jua ya kwamba hakuna Mungu  
anayefaa kuabudiwa kwa haki  
isipokuwa Mwenyezi Mungu, na omiba  
maghufira kwa dhambi zako).  
(Muhammad: 19).

Hakika kaanza na Ilimu. Na kauli ya  
ujinga kwa hakika hayamnufaishi  
mwenye nayo bali ni hasara kwake na  
upotovu juu yake siku ya kiyama,  
**hapana budi atangulize kujifundisha**  
**kabla ya yake Tukufu:** (Na omiba  
**maghufira**) hii ndio Amali, Akaanza  
Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa Elimu  
kabla ya amali; kwa sababu matendo  
yakiwa niya kijinga hakika  
hayamnufaishi mwenye nayo, Aanze

mwanaadamu na Elimu kwanza kisha afanye yale aliyo jifundisha, huu ndio msingi wa dini ya uislam.

Utangulizi:

Kila sifa kamilifu niza Mwenyezi Mungu muumba wa vitu vyote sala na amani ziwe juu ya kipenzi cha Allah mtume wetu Muhammad (s.a.w) ambae ametuwa akiwa nirehma kwa walimwengu wote akiwa nimwenye kubashiri pepo na kukhpfisha moto, na ziwe juu ya maswahaba zake wote waongofu na wote watakao fuata muongozo wake mpaka siku ya qiyama.

Kitabu hiki ni muendelezo wa sehemu ya kwanza ya kitabu kilicho tangulia

tukiwa tunaendelea kunufaika na maneno alio andika imamu Imamu Sheikh Saleh bin Fauzan Al-Fawzan. Mwenyezi Mungu amhifadhi.

**RISALA YA TATU MAMBO**  
**MATATU NI LAZIMA MUISLAM**  
**AJIFUNDISHE NA AYAFANYIE**  
**KAZI .**

Tambua Mwenyezi Mungu akurehemu ya kwamba nilazima juu ya kila Muislam wa Kiume na Wakike kujifundisha mambo haya matatu na kuyafanyia kazi.

**TAMBUA:** ni neno ambalo huletwa kwaajili ya umuhimu wa kinacho elezwa baadae, **na maana yake:**

jifundishe na ufahamu na uwe na yakini.

## MWENYEZI MUNGU

**AKUREHEMU:** Hii ni dua kwako ya rehma, na hili pia limekwisha tangulia kwamba mwalimu yatakiwa awe mpole kwa mwanafunzi, na amuombee dua na kumuhimiza, kwa sababu haya nikatika njia bora za kufundisha, na wala haifai kwake kumkabili kwa ukali na uzito na chuki, kwa sababu haya nanapelekea achulie Elimu, pia yaonyesha nasaha ya mwanachuoni, na kwamba yeye anachotaka ni nasaha na kuelekeza na usawa.

**NI LAZIMA:** Yaonyesha kwamba jambo hili siyo hiyari, anaetaka

anafanya na asietaka anaacha, bali ulazima hapa ni katika namna ya mkazo kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na siyo ulazima kutoka kwa mwanachuoni, bali ni kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa yale aliyo yateremsha katika Kitabu na Sunna, katika kuwalazimisha waja kwa mambo haya.

**NI LAZIMA JUU YA KILA**  
**MUISLAM WAKIUME NA**  
**WAKIKE,**

Maana yake: ni lazima juu yakila mwanamume na mwanamke miongoni mwa Waislam sawasawa wakiwa huru au watumwa au wanaume au wanawake, kwa sababu mwanamke

hushirikiana na mwanaume kwenye mambo ya lazima mengi sana, isipokuwa yale yanayo wahusu wanaume pekeyao kwa dalili inayo wahusu wao tu, **mfano:** ulazima wa swala za jamaa misikitini, swala za ijumaa, na mfano wa kuzuru makaburi mambo haya ni haswa kwa wanaume, na mfano wa kupigana Jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu, sababu jambo hili ni maalumu kwa wanaume.

## MAMBO MATATU :

Kujifundisha maana yake hapa: kupata elimu kutoka kwa wanachuoni na kuhifadhi na kufahamu na kudiriki mambo sawasawa, hii ndiyo elimu,

nawala siyo makusudio kujisomea tu ovyo au kutwalii tu.

Na haifai kujifundisha kwenye vitabu kama hali ya zama tulizo nazo, kwa sababu kujifundisha kwa kutumia vitabu ni hatari sana, hupatikana madhara makubwa, na kufundishana - kwanjia hiyo ya vitabu- kuna dhuru zaidi kuliko mjinga; kwa sababu mjinga anatambuwa kama yeye ni mjinga na husimama kwenye kiwango chake, lakini mwenye kujifundisha hujiona ya kwamba ni mjuzi, ana halalisha aliyo ya haramisha Mwenyezi Mungu, na ana haramisha aliyo ya halalisha Mwenyezi Mungu, na anaongea na husema juu ya

Mwenyezi Mungu bila ya elimu, ni mambo hatari sana.

Elimu haichukuliwi kutoka kwenye vitabu moja kwa moja, isipokuwa vitabu ni nyenzo tu, lakini uhakika wa elimu huchukuliwa kutoka kwa wanachuoni ambao wapo katika njia ya wema walio tangulia vizazi kwa vizazi, na vitabu ni nyenzo za kutafutia elimu.

## KUAMINI YA KWAMBA:

A. MWENYEZI MUNGU  
AMETUUMBAA.

B. ANATURUZUKU.

C. HAKUTUACHA  
BURE

Mwenyezi Mungu ametuumba na kuturuzuku na hajatuacha bure.

1:kwamba Mwenyezi Mungu ametuumba, **maana yake:** Ametuweka baada ya kuto kuwepo, sisi kabla yakutuumba hatukuwa chochote, **kama alivyo sema Mwenyezi Mungu Mtukufu:** (Hakika ulimpitia binaadamu kipindi katika zama ambacho kwamba hakuwa kitu kinachoweza kutajwa). (**Al-Insaan: 1**).

Na akasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: (**Akasema:** Ndio hivyo hivyo amesema Mola wako: Haya ni rahisi kwangu. Na hakika Mimi nilikwisha kukuumba wewe zamani na hali hukuwa kitu).

(Maryam: 9).

Alikuwa binaadamu kabla ya kuumbwa si chochote, ambae kamuweka na kumuumba ni Mwenyezi Mungu Mtukufu, **amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:** (Au wao wameumbwa pasipo kutokana na kitu chochote, au ni wao ndio waumbaji?). (Tuur: 35).

2:Na kuturuzuku: Tulipokuwa niwenye kuhitajia rizki chakula kinywaji mavazi nyumba vipando na mazuri, alitambua Mwenyezi Mungu Mtukufu shida zetu akawepesisha vilivyoko mbinguni na aridhini vyote kwa masilahi yetu kwaajili tubakie kwenye uhai, na kwaajili ya kuvitumia ili

tufanye lengo la kuumbwa kwetu, nalo ni Ibada ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

3:Na hakutuacha bure: ni kitu kilicho achwa ambacho hakina faida yoyote, Mwenyezi Mungu ametuumba na kuturuzuku kwa hikma, hakutuumba kwa mchezo wala bure, amesema **Mwenyezi Mungu Mtukufu:** (Je! Mlidhani ya kwamba tuli kuumbeni bure na yakwamba nyinyi kwetu hamtarejeshwa?). (Al-Muuminun: 115).

Na akasema Mwenyez Mungu Mtukufu: (**Ati anadhani mwanadamu kuwa ataachwa bure?\*** Kwani hakuwa yeye ni tone ya manii lilio shushwa?\*

Kisha akawa pande la damu, tena Mwenyezi Mungu akamuumba na akamtengeneza vilivyo). (Al-Qiyamah: 36-38).

Na akasema: (Na hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yao bure. Hiyo ni dhana ya walio kufuru. Ole wao walio kufuru kwa Moto utakao wapata). (**Swaad:** 27).

Mwenyezi Mungu ametuumba na katuumbia hizi rizki na yanayo wezekana kwa hikma kubwa na lengo nzuri, nalo ni kumuabudu Mwenyezi Mungu Mtukufu, na wala hakutuumba kama wanyama ambao wameumbwa kwa maslahi ya viumbe kisha vinakufa na kuondoka; kwa sababu havija

kalifishwa wala kuamrishwa wala kukatazwa, kwa hakika Ametuumba kwaajili ya ibada yake, **kama alivyo sema Mwenyezi Mungu Mtukufu:** (Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu **Mimi\*** Na sitaki kwao riziki, wala sitaki wanilishe\* Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kuruzuku, Mwenye nguvu, **Madhubuti**). (Adh-Dhaariyaat: 56-58).

Wala hakutuumba kwaajili ya maisha ya dunia tu, ili tuishi ndani yake, tukeshe tucheze, na tule na tunywe, tujitanue ndani yake kisha pisiwe na chochote, na kwa hakika maisha ni shamba, na sokoni ni nyumba ya akhera, tunajiandaa kwa matendo mema, kisha tunakufa na

tunaelekea huko, kisha tunafufuliwa,  
kisha tuna hesabiwa na tunalipwa kwa  
matendo yetu.

Haya ndio makusudio ya kuumbwa  
majini na watu, na ushahidi wa hayo ni  
mwingi sana wakuonyesha kufufuliwa  
na malipo na hesabu, na akili  
inaonyesha hili, kwa sababu  
haiwezekani kwa hikma ya Mwenyezi  
Mungu Mtukufu kuumba kiumbe  
waajabu, na akaufanya huu ulimwengu  
kwaajili ya binadamu kisha awaache  
wafe waondoke bila faida. Huu ni  
mchezo, hapana budi kujulikana  
majibu ya matendo katika nyumba ya  
akhera.

Kwa hili kuna baadhi ya watu wanao maliza umri wao katika Ibada ya Mwenyezi Mungu na katika kumtii yeye, hali ya kuwa yupo katika ufakiri na shida, na huenda akawa ni mwenye kudhulumiwa kubanwa kuonewa na wala asilipiwe katika hii dunia, na kinyume chake, unakuta mwengine kafiri hamuamini Mungu na ni muovu lakini amekunjiliwa ana furaha katika hii dunia, ana neemeka amepewa anayo yataka, anafanya aliyo haramisha Mwenyezi Mungu, anawadhulumu waja anawafanyia vibaya, anakula mali zao, anaua bila haki, anawasaliti watu anajinyanyuwa kisha anakufa katika hali hiyo, hakupata chochote katika adhabu.

Je! Yafaa kwa uadilifu wa Mwenyezi Mungu Mtukufu na hekima zake amuache huyu mtiifu bila malipo?, na amuwache huyu kafiri bila kumlipa?, jambo hili halifai kutokana na Uadilifu wa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Kwa sababu hiyo kajaaliya nyumba ya akhera aliye fanya wema kulipwa kwa wema wake, na aliye fanya mabaya kwa mabaya yake, patadhihirika matunda ya matendo.

Dunia ni nyumba ya matendo, lakini akhera yao ni nyumba ya malipo, ima pepo au moto, na hakutuacha bure kama wanavyo dhani wasio muamini Mwenyezi Mungu na wanao amini uhai wa dunia bila akhera, [amesema](#)

**Mwenyezi Mungu Mtukufu:** (Na walisema: Hapana isipokuwa huu uhai wetu wa duniani tunakufa na tunaishi, na hapana kinacho tuhiliki isipokuwa zama. Lakini wao hawana ilimu ya hayo, isipokuwa wao wanadhani tu). (Al-Jaathiyah: 24).

Haya ndio maneno ya wasio muamini Mwenyezi Mungu ambao hawaamini kufufuliwa.

**Na kwa hakika Mwenyezi Mungu kawakanusha Akasema:** (Kwani tutawafanya Waislamu mfano wa wakosefu?\* Mna nini? Mnahukumu vipi?). (Al-Qalam: 35-36).

**Na akasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:** (Je! Wanadhani wanao tenda

maovu kuwa tutawafanya kama walio amini, na wakatenda mema, sawa sawa uhai wao na kufa kwao? Ni hukumu mbaya wanayo ihukumu!). (Al-Jaathiyah: 21).

Na akasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Ama! Tuwajaalie walio amini na wakatenda mema kama wafanyao uharibifu katika ardhi? Au tuwajaalie wachamungu kama waovu?). (Swaad: 28).

Hili haliwezekani na wala haliwi.

**BALI KATUTUMIA MITUME.**

Ilivyokuwa Ibada haifai tuichukue kutoka kwa Fulani na Fulani tutakao

waona wazuri, au kumuiga Fulani na Fulani katika wanadamu, katutumia **Mwenyezi Mungu Mitume** watubainishie Namna tutakavyo muabudu; kwa sababu Ibada ni kitu rasmi, na haifai kumuabudu **Mwenyezi Mungu** kwa chochote isipokuwa kwa aliyo amrisha.

Ibada ni kitu rasmi juu ya yale walio kujanayo **Mitume (s.a.w)**, na hekima ya kutumwa **Mitume** ili wawabainishie watu namna watakavyo muabudu **Mungu** wao, na wawakataze shirki na kumkufuru **Mwenyezi Mungu Mtukufu**.

Hii ndiyo kazi ya **Mitume (s.a.w)**, kwa sababu hii anasema **Mtume (s.a.w)**:

(Yeyote atakae zuwa katika dini yetu mambo ambayo hayapo atarejeshwa mwenyewe).

Kapokea hadithi hii Imam Bukhari kabla ya hadithi (7350), na Muslim (18/1718), hadithi ya Bibi Aisha (s.a.).

Ibada ni kitu rasmi, na bida'a ni yenye kurejeshwa, na mambo yasio faa ni yenye kurejeshwa, na kufuata kama kipofu imekatazwa. Ibada hazichukuliwi isipokuwa katika sheria alio kujanayo Mtume (s.a.w).

## BALI KATUTUMIA MTUME :

Nae ni Muhammad (s.a.w) mwisho wa manabii, amemtuma ili atubainishie kwa nini Ametumba? Na atubainishie

namna ya kumuabudu Mwenyezi  
Mungu Mtukufu, na atukataze  
ushirikina na ukafiri na maasi, hii ndio  
kazi ya Mtume (s.a.w) na amefikisha  
kwa uwazi, na akatekeleza amana, na  
akaunasihi Umma (s.a.w), na  
akabainisha na akaweka wazi, na  
akatuacha katika njia nyeupe usiku  
wake ni kama mchana wake, yegetto  
atacae kwenda kinyume ataangamia,  
**kama ilivyo katika maneno yake**  
**Mwenyezi Mungu Mtukufu:** (Leo  
nimekukamiliishieni Dini yenu, na  
nimekutimizieni neema yangu, na  
nimekupendeleeni Uislamu uwe ndiyo  
Dini).

(Al-Maaida: 3).

## **YEYOTE ATAKAE MTII ATAINGIA PEPONI, NA YEYOTE ATAKAE MUASI ATAINGIA MOTONI.**

Atakae mtii, **maana yake:** kwa yale aliyo amrisha ataingia Peponi, na atakae muasi, **maana yake:** kwa yale aliyo kataza ataingia Motoni.

Ukweli wa haya ni mwingi ndani ya Qur-ani, **kama alivyo sema Mwenyezi Mungu Mtukufu:** (Mwenye kumti'i Mtume basi kwa hakika ndio amemti'i Mwenyezi Mungu). (An-Nisaa: 80).

**Na akasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:** (Na mkimtii yeye mtaongoka). (An-Nuur: 54).

Na akasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Na mtiini Mtume, ili mpage kurehemewa). (An-Nuur: 56).

Yeyote atakae mtii ataongoka na ataingia Peponi, na yeyote atakae muasi atapotea na ataingia Motoni, amesema Mtume (s.a.w): (Nyoote mtaingia Peponi isipokuwa Yule atakaekataa, **wakasema**: ni nani atakae kataa ewe Mtume? Akasema: Yeyote atakae nitii Mimi ataingia Peponi na yeyote atakae niasi Mimi huyo ndiyo alie kata).

Kapokea hadithi hii Imam Bukhari (7280). hadithi ya Abaa huraira (s.a.).

Kauli yake Mtume (s.a.w): ATAKAE KATAA, **maana yake**: Amekataa

kuingia Peponi. Na akasema Mtume (s.a.w): (Hato nisikia mimi yahudi au mkristo kisha hakuamini yale niliyo kujanayo isipokuwa ataingia Motoni).

Kapokea hadithi hii Imam Muslim (153), hadithi ya Abaa huraira (ع.ا).

Yeyote atakae mtii ataingia peponi na yeyote atakae muasi ataingia motoni, na hii ndio tofauti kati ya muislamu na kafiri.

Na dalili kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Hakika Sisi tumemtuma kwenu Mtume aliye shahidi juu yenu kama tulivyo mtuma Mtume kwa Firauni\* Lakini Firauni alimuasi huyo Mtume, basi tukamkamata mkamato wa mateso). (Al-Muzammil: 15-16).

Na dalili, **maana yake**: juu ya kutumwa Mitume kauli yake Mwenyezi Mungu **Mtukufu**: (**Hakika Sisi tumemtuma kwenu Mtume aliye shahidi juu yenu kama tulivyo mtuma Mtume kwa Firauni\*** Lakini Firauni alimuasi huyo **Mtume**, basi tukamkamata mkamato wa mateso).

Na maana ya: Tumemtuma: tumemtumia na tumemfunulia.

**KWENU**: Enyi makundi aina mbili majini na watu, ni maneno kwa watu wote; kwa sababu ujumbe wa Nabii Huyu unaenea watu wote hadi kusimama kiyama .

**MTUME**: ndie Muhammad (**s.a.w**).

**SHAHIDI JUU YENU:** maana yake:  
mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu  
siku ya kiyama kama yeye  
kakufikishieni ujumbe wa Mwenyezi  
Mungu na hoja ikasimama juu yenu,  
**kama alivyo sema Mwenyezi Mungu**  
**Mtukufu:** (Mitume hao ni wabashiriaji  
na waonyaji, ili watu wasiwe na hoja  
juu ya Mwenyezi Mungu baada ya  
kuletewa Mitume. Na Mwenyezi  
Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye  
hikima). (**An-Nisaa: 165**).

Asitokee yejote siku ya kiyama  
akasema: mimi sijui kama nimeumbwa  
kwaajili ya Ibada, mimi sijui yepi ni  
lazima kwangu, na sijui yepi ni haramu  
kwangu, haiwezekani akasema haya,  
kwa sababu Mitume (**s.a.w**)

wamekwisha wafikishia, na huu  
Umma wa Muhammad (s.a.w)  
utashuhudiya juu yao, kama alivyo  
sema Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Na  
vivyo hivyo tumekufanyeni muwe  
Umma wa wastani, ili muwe  
mashahidi juu ya watu, na Mitume awe  
ni shahidi juu yenu). (Al-Baqara: 143).

Umma huu utakuwa ni shahidi juu ya  
nyumati zilizo tanguliya siku ya  
kiyama kwamaba Mitume wao  
wamewafikishia ujumbe wa Mwenyezi  
Mungu, kwa yale walio yakuta ndani  
ya kitabu cha Mwenyezi Mungu  
Mtukufu, kwa sababu Mwenyezi  
Mungu katusimulia habari za nyumati  
zilizo tanguliya na Mitume na walio  
yasema kwa nyumati zao.

Yote hayo tumeyajua kupitia kitabu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu kitabu ambacho Hautakifika upotovu mbele yake wala nyuma yake, kimeteremshwa na mwenye hikima, msifiwa.

**NA ATAKUWA MTUME:** Nae ni Muhammad ([s.a.w](#)), atakuwa ni shahidi juu yenu Ummati Muhammad, atashuhudia juu yenu mbele ya Mwenyezi Mungu kwamba yeye amesimamisha juu yenu hoja, na akafikisha kwenu Ujumbe, na akakupeni nasaha kwaajili Mwenyezi Mungu, [hapatakuwa na hoja kwa yejote siku ya kiyama kwa kusema:](#) sikufikiwa na chochote, sikufikiwa na muonyaji, hadi makafiri Watakiri

wakati watakapo tupwa motoni,  
amesema **Mwenyezi Mungu Mtukufu:**  
(Kila mara likitupiwa kundi humo  
walinzi wake huwauliza: Kwani  
hakukujieni mwonyaji? Watasema:  
Kwani! Ametuijia mwonyaji, lakini  
tulimkadhibisha, na tukasema:  
**Mwenyezi Mungu hakuteremsha**  
chochote. Nyinyi hamumo isipokuwa  
katika upotovu mkubwa!). (**Al-Mulk:**  
**8-9).**

Wanasema kwa Mitume: Nyinyi mpo  
katika upotovu, wao  
wanawakadhibisha Mitume na  
kuwafanya ni wapotovu .

Hii ndio hikima ya kutumwa Mitume;  
kwaajili ya kusimamisha hoja kwa

waja, na muongozo kwa yule anaetakiwa na Mwenyezi Mungu uongofu, Mwenyezi Mungu huwaongoza waja wake awatakao kupitia mitume, na husimamisha hoja juu ya wenyе kupinga na kukanusha na kukufuru.

**KAMA TULIVYO MTUMA  
MTUME KWA FIRAU NI:** Mtume: ni Nabii Mussa (*s.a.w*), na Firauni ndie mfalme jeuri wa Misri, ambae alidai Uungu, **na Firauni:** ni jina la kubandikwa kila anae tawala Misri huitwa Firauni. **Makusudio hapa ni Firauni alie dai Uungu:** (Akasema: *Mimi ndiye Mola wenu mkuu kabisa*). (**An-Naziat:** 24).

**LAKINI FIRAUNI ALIMUASI HUYO MTUME:** Huyo ni Nabii Mussa (**s.a.w**), alipingwa na Firauni kama alivyo simulia Mwenyezi Mungu katika kitabu chake yaliyo tokea kati ya Nabii Mussa na Firauni, na alipo fikia Firauni na watu wake.

**BASI TUKAMKAMATA, Maana yake:** Tulimkamata Firauni kwa adhabu, **nayo:** hakika Mwenyezi Mungu alimzamisha yeye na watu wake ndani ya bahari kisha akawaingiza motoni: (**Basi kwa ajili ya makosa yao waligharikishwa wakaingizwa Motoni**). (Nuuh: 25).

Akawa katika moto katika barzakhi  
**(Kaburini)**, Amesema Mwenyezi  
Mungu mtukufu :

(Wanaonyeshwa Moto asubuhi na  
jioni). (Suuratul Ghaafir 46.)

Adhabu hii itakuwa kaburini kabla ya akhera,wataonyeshwa motoni asubuhi na jioni,yaani kuchomwa namoto mpaka kitakapo simama kiyama,na huu niushahidi tosha wakuthibitisha kuwepo kwa adhabu kaburini,Allah atukinge, Allah anasema:

)Na itapo fika Saa ya Kiyama  
patasemwa: Waingizeni watu wa Firauni katika adhabu kali kabisa!)  
**(Suuratul Ghaafir 46).**

## ADHABU TATU ZA WATU WA FIRAUN:

1-Hakika mwenyezi mungu  
aliwazamisha na kuwapoteza  
kwamuda mmoja.

2-Hakika wao wana adhibiwa Katika  
makaburi yao mpaka kitakapo simama  
kiyama.

3-Watakapo fufuliwa siku yakiyama  
wataingia katika adhabu kali, Allah  
atukinge.

Vilevile yejote atakae muasi mtume  
(s.a.w) hakika mafikio yake yatakua  
katika adhabu kali kuliko Firauni,  
kwasababu mtume Muhamad (s.a.w) ni  
mtume bora kuliko mitume walio pita,

atakae muasi adhabu yake inakuwa kubwa zaidi.

Mwenyezi mungu anasema kuhusu firauna: (**basi tukamshika mshiko wa mateso**).

Yaani kwa ukali na nguvu bila ulaini ndani yake.

Anasema Mwenyezi Mungu katika surati Hudi: { **Na ndio kama hivyo ndivyo inavyo kuwa Mola wako Mlezi anapo ikamata miji inapo kuwa imedhulumu. Hakika mkamato wake ni mchungu na mkali.** }

( Hudi 102).

Aya hii ni ushahidi tosha juu ya neema ya Mwenyezi mungu juu yetu kwa

kumtuma mtume Muhamad (s.a.w) kwetu na hakika lengo la kumtuma ni kutubainishia njia sahihi ya kufanya ibada, yoyote atakae mtii ataingia peponi, na yoyote atakae muasi ataingia motoni, kama alivyo ingia firauni na watu wake motoni, pindi walipo muasi Nabii Mussa (a.s), vilevile maadui wa mitume wote hii ndio njia yao.

Mwenyezi Mungu mtukufu haridhii kushirikishwa nayoyote katika ibada.

### **MAS'ALA YA PILI:**

Hakika Mwenyezi Mungu haridhii kushirikishwa na yoyote katika ibada.

Haya mas'ala yanaambatana na  
mas'ala ya kwanza, kwa kuwa ya  
kwanza:

Yanabainisha uwajibu wa kumuabudu  
Mwenyezimungu na kumfuata mtume  
(s.a.w), na ndio maana ya shahada  
mbili, shahada ya (Lailaha ila Allah  
Muhamadu rasulu Allah).

Na mas'ala yapili: Nikwamba ibada  
inapo changanyika na ushirikina  
haikubaliwi, kwasababu ni lazima iwe  
ibada kwaajili ya Mwenyezi Mungu  
mshindi mtukufu.

Yoyote atakae muabudu Mwenyezi  
Mungu akamshirikisha na kitu kingine  
ibada yake inakuwa batili, kuwepo  
ibada hiyo na kuto kuwepo ni sawa,

kwasababu ibada haifai bila ikhlas na kumpwekesha Mwenyezi Mungu, pindi zitakapo changanyika na ushirikina zitaharibika, **kama alivyosema Mwenyezi Mungu mtukufu:** { Na kwa yakini yamefunuliwa kwako na kwa walio kuwa kabla yako: Bila ya shaka ukimshirikisha Mwenyezi Mungu a'mali zako zitaanguka, na lazima utakuwa mionganoni mwa wenye kukhasiri}.(Azzumar 65).

Na amesema Mwenyezi Mungu mtukufu:

{Na lau wangeli mshirikisha yangeli waharibikia waliyo kuwa wakiyatenda}(An'aam-88).

Ibada haiwezi kuitwa ibada ila ikiwa ni kwalengo la kumpwekesha Mwenyezi Mungu (**tauhiidi**), kama ilivyo swala haiwezi kuitwa swala mpaka uiswali ukiwa msafi (twahara.)

Ikichanganywa swala na kinacho tengua udhu basi kinaiharibu swala na kuibatilisha, ndio maana unakuta Mwenyezi Mungu anakusanya katika aya nyingi baina ya kuamrisha watu wafanye ibada na anawakataza shirki.

Alisema Mwenyezi Mungu:{ Muabuduni Mwenyezi Mungu wala msimshirikishe na chochote }.(**An-Nisaai-36**).

Alisema Mwenyezi Mungu { Nao hawakuamrishwa kitu ila wamuabudu

Mwenyezi Mungu kwa kumtakasia Dini, wawe waongofu, na washike Sala, na watoe Zaka. Na hiyo ndiyo Dini madhubuti }. (Al-bayyinah 5).

Na alisema Mwenyezi Mungu: { Na hatukumtuma kabla yako Mtume yejote ila tulimfunulia ya kwamba hapana mungu isipo kuwa Mimi. Basi niabuduni Mimi tu }. (Anbiyaa 25).

Mwenyezi Mungu kusema: { hapana mungu isipo kuwa Mimi. }

Kunamambo mawili:

1- kukanusha ushirikina.

2-kuthibitisha ibada kwa Mwenyezi Mungu mtukufu pekeyake.

Na alisema Mwenyezi Mungu  
mtukufu: {Na Mola wako Mlezi  
ameamrisha kuwa msimuabudu yeyote  
ila Yeye tu}. (Sura Al Israai23)

}Na kwa hakika kwa kila umma  
tuliutumia Mtume kwamba:  
Muabuduni Mwenyezi Mungu, na  
muepukeni Shetani.} (An Nahl 36).

Amekutanisha baina ya kumuabudu  
Mwenyezi Mungu peke yake na  
kujiepusha na ibada za matwaghuti  
(Mashetani).

Kwasababu ibada ya Mwenyezi  
Mungu haiwi ibada ila ikiwa ni pamoja  
na kujiepusha na matwaghuti, nao ni  
kufanya ushirikina.

Anasema Mwenyezi Mungu mtukufu: {Basi anaye mkataa Shet'ani na akamuamini Mwenyezi Mungu bila ya shaka amekamata kishikio madhubuti, kisicho vunjika. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua.} (Al-Baqara256).

Kumuamini Mwenyezi Mungu peke yake haitoshi mpaka uyakufuru mashetani, na kama siyo hivyo hakika washirikina wanamuamini Mwenyezi Mungu pamoja na kuwa wanamshirikisha.

Anasema Mwenyezi Mungu mtukufu:  
{Na wengi katika wao hawamuamini Mwenyezi Mungu pasina kuwa ni washirikina} (yusuf 106).

Amebainisha Mwenyezi Mungu  
kwamba washirikina  
wanamuamini Mwenyezi Mmungu,  
lakini imani yao wanaiharibu kwa  
kumshirikisha Mwenyezi Mmungu  
katika ibada zao.

Hii ndiyo maana ya kusema: yejote  
mwenye kumuabudu Mwenyezi  
Mungu na akamtii Mtume (**s.a.w**)  
hakika mtu huyo hawezi kumshirikisha  
Mwenyezi Mmungu na chochote,  
kwasababu Mwenyezi Mungu haridhii  
ashirikishwe na chochote katika  
viumbe vyake.

Kutoka kwa abuu huraira (**s.a**) alisema:  
alisema Mtume (**s.a.w**) katika yale  
anayo yapokea kutoka kwa Mola wake

mshindi mwenye nguvu: (Alisema Mwenyezi Mungu mtukufu: Mimi ndio tajiri wa washirika kwa ushirikina wanao ufanya, mwenye kufanya ibada yoyote akamshirikisha katika ibada hiyo asiyekuwa mimi basi nitamuacha na ushirikina wake). Amepokea hadithi hii imamu Muslim (2985).

Kuna watu wanaswali na wanashahidilia kuwa hapana Mola apasae kuabudiwa kwa kahi ila Mwenyezi Mungu, na Muhamad (s.a.w) ni mjumbe wa Mwenyezi Mungu, na wanakithirisha kusema hivyo, na wanafunga na wanahiji, lakini wanayaomba makaburi, na wamuabudu Imamu Hassan na Husein, na Albadawiy, na Fulani na Fulani,

Na wanaomba nusura kwa watu walio kufa, hao ndio ibada zao nibatili, kwasababu wao wanamshirikisha Mwenyezi Mungu mshindi mwenye nguvu, wanachanganya ibada na ushirikina, basi ibada zao ni batili, na nizenye kuporomoka, mpaka watakapo mpwekesha Mwenyezi Mungu mshindi mwenye nguvu, na wamtakasie utii Mwenyezi Mungu na waache kuabudu kisichokuwa Mwenyezi Mmungu.

Na kama siyo hivyo hawatakuwa na chochote, basi ni wajibu kuzinduka kwa hilo, kwasababu Mwenyezi Mungu haridhii kushirikishwa na chochote katika ibada yake kwa vyovyyote atakavyo kua.

Mwenyezi Mungu haridhii kushirikishwa na yeote atakavyo kua, ili asiseme yeote: mimi nachukua kwa watu wema, na watu wazuri uombezi, mimi siabudu masanamu wala mizimu kama ilivyokua enzi za ujinga, mimi nawafanya hawa ni waombezi wangu na siwaabudu.

Tunamuambia kuwa: hayo ni maneno ya watu wa zama za ujinga waliwafanya waombezi wao kwa Mwenyezi Mungu kwasababu ni watu wema, na ni mawalii katika mawalii wa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu haridhii hayo.

Sio kwa malaika alie karibu na  
Mwenyezi Mungu wala Mtume aliye  
tumwa na Mwenyezi Mungu.

Malaika aliye karibu na Mwenyezi  
Mungu ni malaika bora, kama jibrilu  
amani ziwe juu yake, na malaika  
wanao ibeba arshi ya Mwenyezi  
Mungu, na malaika walio karibu nao,  
na malaika walio karibu na Mwenyezi  
Mungu mtukufu.

Pamoja na ukaribu na Mwenyezi  
Mungu na ukaribu wa waja wa  
Mwenyezi Mungu, na daraja kwa  
Mwenyezi Mungu, laiti  
angemshirikisha pamoja na asiye kuwa  
Mwenyezi Mungu pamoja na  
Mwenyezi Mungu katika ibada hakika

Mwenyezi Mungu haridhii kushirikishwa pamoja nae malaika alie karibu na Mwenyezi Mungu, wala Nabii aliye tumwa, kama Muhamad (s.a.w).

Na Nabii Issa na Nuhu na Ibrahim ambao ni Mitume walio pewa sheria, au walio tumwa kwa watu wote, au walio thibiti katika utume wao.

Mwenyezi Mungu haridhii ashirikishwe na yoyote, hata kama atakua ni mbora wa malaika, au ni mbora wa watu.

Yeye Mwenyezi Mungu haridhii ashirikishwe na yoyote katika malaika, au katika mitume, itakuaje kwa viumbe wasio kuwa mitume na malaika

miongoni mwa watu wema na mawalii walio wema!

Basi wasio kuwa malaika na mitume ndio kabisa, hawezi Mwenyezi Mungu kumridhia kwa kumshirikisha pamoja nae kitu kingine, katika ibada.

Na haya ni majibu ya wale ambao wanao dai kwamba wao wanawafanya wale wema walio pita na mawalii uombezi kwa Mwenyezi Mungu ili awakurubishe hao kwa Mwenyezi Mungu, **kama walivyo sema:** {Sisi hatuwaabudu ila wapate kutujongeza tu kumkaribia Mwenyezi Mungu} **(Azzumar3).**

Na kama siyo hivyo hakika wao wanaitakidi kwamba hao hawaumbi

wala hawatoi rizki na hawamiliki kifo  
wala uhai wala kufufuka, bali  
makusudio yao ni kupata mtu wa  
katikati ili awaombee kwa Mwenyezi  
Mungu mshindi mwenye nguvu,  
kwasababu hiyo waliwafanyia ibada  
kwa lengo la kujikurubisha kwao,  
walichinja kwaajili ya makaburi, na  
wakatoa nadhiri kwa ajili ya ibada, na  
wakaomba nusra na kuwaita walio  
kufa.

Na ushahidi ni kauli ya Mwenyezi  
Mungu mtukufu: { Na hakika misikiti ni  
ya Mwenyezi Mungu, basi  
msimuabudu yejote pamoja na  
Mwenyezi Mungu }  
(Al-Jinn 18).

Mwenyezi Mungu haridhii kushirikiana na yeote atakavyo kua, na haya yametajwa wazi katika Qur'an, na Sunna za Mtume Muhamad (**s.a.w**), lakini yeote ambae hakuwa na akili wala mazingatio, na kuacha kufuaata mtu kipofu, na kuleta sababu ambazo ni batili, na azinduke na nafsi yake.

Na ushahidi kua Mwenyezi Mungu haridhii kushirikishwa na yeote, **ni kauli ya Mwenyezi Mungu mtukufu:** {Na hakika misikiti ni ya Mwenyezi Mungu, basi msimuabudu yeote pamoja na Mwenyezi Mungu} (Al-Jinn 18)

Misikiti ni nyumba za Mwenyezi Mungu, na ni sehemu zilizo andaliwa

kwa ajili ya swala, nazo ni sehemu zinazo pendwa zaidi kwa Mwenyezi Mungu, nazo ni nyumba ameidhinisha Mwenyezi Mungu zinyanyuliwe na litaje jina la Mwenyezi Mungu, na inapaswa iwe misikiti hii ni sehemu ya ibada ya Mwenyezi Mungu pekeyake, na kisitokee chochote katika misikiti ambacho ni cha kumshirikisha Mwenyezi Mungu, yasiwekwe ndani yake makaburi, kwasababu mtume (s.a.w) amemlaani mwenye kufanya kitendo hicho, na akaeleza kuwa kufanya hivyo ni kitendo cha mayahudi, na manaswara, na akatukataza kufanya hivyo mwisho wa uhai wake akiwa katika wakati wa kutolewa roho yake akisema: kutoka kwa Jundabi bin Abdillah albajaliy

(﴿.a) alisema: alisema Mtume (s.a.w):

"Fahamuni hakika walio kuwa kabla  
yenu walikua wakiyafanya makaburi  
ndio misikiti basi fahamuni msilifanye  
kaburi langu kua msikiti hakika mimi  
nawakataza hilo" Imepokelewa na  
Muslim (532)

alikuwa akiyasema haya akiwa katika  
wakati wa kutolewa roho yake.

Na kutoka kwa Aisha (﴿.a) alisema:

alikuwa akisema Mtume (s.a.w)

"Laana za Mwenyezi Mungu ziwe juu  
ya mayahudi na manaswara  
waliyafanya makaburi ya mitume wao  
kuwa ni misikiti" Ameipokea na  
Bukhari (435,436) na Muslim(531).

Misikiti inatakiwa itwaharishwe kutokana na athari za ushirikina na mizimu, na yasisimamiwe makaburi kwa kuyatukuza, au kujajengea, bali misikiti ifanywe ni sehemu za ibada ya Mwenyezi Mungu peke yake, isimamishwe ndani yake swala, na litajwe jina la Mwenyezi Mungu ndani yake, na kisomwe ndani yake kitabu cha Mwenyezi Mungu, na ziwekwe ndani yake darsa mbalimbali zenye manufaa, na watu wakae itikafu kwaajili ya kufanya ibada, huu ndio wadhfa wa misikiti.

Ama kusimamishwa msikitini mizimu inayo abudiwa kinyume cha Mwenyezi Mungu, basi hiyo sio misikiti, na kufanya hivyo ni ushirikina hata kama

wenye misikiti hiyo wataiita kua ni  
misikiti, **kwa sababu Mwenyezi**  
**Mungu anasema:** {Na hakika misikiti  
ni ya Mwenyezi Mungu.}...

Yaani misikiti siyo ya kisichokua  
Mwenyezi Mungu, na kwakuwa  
misikiti ni sehemu ya mkusanyiko wa  
watu, basi inatakiwa iwe ni sehemu  
twahara kutokana na ushirikina, na  
uzushi, na mambo yasiyo kubalika  
kisheria, kwasababu watu wanapata  
elimu na wanafanya ibada katika  
misikiti, pindi watakapo kuta katika  
misikiti ushirikina au mambo yasio faa  
kisheria huenda wakaathirika nayo au  
wakayachukua na kuyatangaza duniani  
kote, Kwahiyo ni wajibu iwe misikiti

ni yenye kutwaharishwa kutokana na ushirikina.

Na mionganini mwa misikiti mitukufu kulio yote ni msikiti mtukufu wa Makkah, kama alivyo amrisha Mwenyezi Mungu alie tukuka alie wa juu utwaharishwe, alisema Mwenyezi Mungu mtukufu:

{Na pale tulipo muweka Ibrahim pahala penye ile Nyumba tukamwambia: Usinishirikishe na chochote; na isafishe Nyumba yangu kwa ajili ya wanao izunguka kwa kut'ufu, na wanao kaa hapo kwa ibada, na wanao rukuu, na wanao sujudu} (Hajj 26).

Mwenyezi Mungu aliutwaharisha kutokana na nini? aliutwaharisha kutokana na ushirikina na uzushi na mambo yasiyo kubalika katika dini kama alivyo utwaharisha kutokana na na najsi au uchafu wa takataka.

Msiombe enyi watu pamoja na Mwenyezi Mungu yeyote, msiombe nusra kwa yoyote pamoja na Mwenyezi Mungu, **kama vile kusema:** ewe Mwenyezi Mungu, ewe Muhammad, ewe Mwenyezi Mungu, ewe Abdul Qadir, au kusema: ewe Abdul Qadir, ewe Muhamad, au mfano wa hayo, hakika Mwenyezi Mungu haridhii hayo na hayakubali.

Hakuna yejote anae toka katika hukumu hiyo hakuna malaika alie karibu na Mwenyezi Mungu, wala mtume alie tumwa na Mwenyezi Mungu, wala sanamu au mzimu, wala kaburi la shekh, au walii, wala aliye kufa, vyovyote atakavyo kuwa.

Qauli ya Mwenyezi Mungu {...basi msimuabudu yejote pamoja na Mwenyezi Mungu} (Al-Jinn 18).

Inakusanya wote wenye kuombwa kinyume cha Mwenyezi Mungu, na Aya hii imeonyesha kuwa ibada haikupi manufaa mpaka uifanye ukiwa na Tauhiidi, na kwa hakika ukiichanganya na ushirikina basi inabatilika, na inakua ni mzigo kwa

**mfanyaji, kisha akasema Mwenyezi Mungu:** {Nahakika misikiti ninyumba za Mwenyezi Mungu...} ni wajibu ijengwe misikiti kwa nia ilio takasika kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na siyo kwa ajili ya kujionyesha, au kutaka asikike, au kwasababu ubaki utajo wake baada ya kufa kama wanavyo sema, au uwe msikiti ni athari za kiislam, kujenga msikiti kwa sababu ya mambo hayo haifai.

Misikiti inajengwa kwasababu ya kufanya ibada, na kwa nia ya kufanya ibada, na iwe nia imetakasika kwa ajili ya Mwenyezi Mungu mwenye nguvu alie tukuka, na misikiti inajengwa kwa lengo la kuchuma thawabu, na haijengwi kwasababu ya kuchuma

haramu, kwasababu misikiti ni ya Mwenyezi Mungu, Kutoka kwa Abii Hurayra (رضي الله عنه) alisema: alisema Mtume (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ): "Na hakika Mwenyezi Mungu hapokei ila kitu kizuri" Imepokelewa na Muslim (1015).

Na misikiti inajengwa kwa pesa ya halali, na iwe niya ya kujenga hiyo misikiti ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu mwenye nguvu aliye tukuka, hataki ingwe kwa sifa za watu au kubakia utajo wa mtu, au kujionyesha au kutaka asikike, hakika kujenga msikiti ni ibada na ibada ni wajibu iwe kwaajili ya Mwenyezi Mungu mshindi na mtukufu.

Ndugu katika imani hii nisehemu ya pili katika kitabu hiki cha Masomo katika umuhimu wa Tawhiid .(2)  
Muhtasari wa kitabu cha Al-Usulu AL-Thalathah cha Imamu Fawzani Allah amuhifadhi tuwe pamoja katika sehemu ya tatu Allah akiipenda .

## **WALAA NA BARAA.**

3.Mwenye kumtii Mtume (s.a.w) na akampwekesha Mwenyezi  
Mungu,haifai kwake kuwapenda wale wenye kumfanyia uadui Mwenyezi  
Mungu na mtume wake hata kama watakuwa niwatu wakaribu zaidi.

Haifai kwa mwenye kumpwekesha  
Mwenyezi Mungu kumpenda mwenye kumfanyia uadui Mwenyezi Mungu na

mtume wake hatakama atakuwa nimtu wakaribu zaidi.

Haya maswala ya walaa na  
baraa(kupenda kwa ajili ya Mwenyezi  
**Mungu** na kuchukia kwajili ya  
**Mwenyezi Mungu**) Nikatika maswala  
ya tauhiidi,pia nikatika haki ya tauhidi  
kuwapenda mawalii wa Mwenyezi  
Mungu,na kuwachukia maadui wa  
**Mwenyezi Mungu.**

Muislam anawapenda wapenzi wa  
Mwenyezi Mungu,yaani hatakiwi  
kupenda ila vipenzi vya Mwenyezi  
Mungu,na awanusuru muislam  
anatakiwa awe karibu na waislam  
wapendane,**kama alivyo sema**  
**Mwenyezi Mungu:**{....Na jamaa wa

nasaba wanastahikiana wenyewe kwa  
wenyewe zaidi katika Kitabu cha  
**Mwenyezi Mungu.... }**(Al Anfaal 75)  
hayawi mapenzi baina ya muislam na  
kafiri,bali yanakuwa baina ya  
waislam,**kama alivyo sema Mwenyezi  
Mungu:**{....wala Mwenyezi Mungu  
hatawapa makafiri njia ya kuwashinda  
Waumini }.(An-Nisaa 141).

Hivyo ndivyo inavyo paswa kwa  
waumini watambulike kwa  
makafiri,haifai kwa yoyote mwenye  
kumpwekesha Mwenyezi Mungu,na  
akamtii mtume **(s.a.w)**kuwapenda  
wenye kumfanyia uadui Mwenyezi  
Mungu.

Na kufanya uaduia maana yake:nimtu  
kua katika upande na Mwenyezi  
Mungu mtukufu na mtume wake kua  
upande mwingine,(yaani wako tofauti).

Maana ya kusema (Hatakama nindugu  
wakaribu):

Yaani katika upande wa nasabu,pindi  
atakapo kua nindugu yako wakaribu  
nimwenye kumfanyia uadui Mwenyezi  
Mungu na mtume wake(s.a.w)niwajibu  
juu yako kumfanyia uadui na kukata  
undugu nae.

Na yoyote atakae kua kipenzi wa  
Mwenyezi Mungu na mtume wake  
(s.a.w) niwajibu juu yako kumpenda  
na umfanye kuwa rafiki yako

hatakama nimtu wako wambali katika  
nasabu,hatakama atakuwa  
nimuejemi(**Mtu asie kuwa wa rangi**  
**yako au lugha yako**) au mweusi,au  
mweupe,au mwekundu, niwajibu  
kwako kumfanya rafiki na kumpenda,  
akiwa niwakutoka katika mji wako au  
niwakutoka mashariki ya mbali,au  
magharibi yambali,**alisema Mwenyezi**  
**Mungu mtukufu:**{ Na Waumini  
wanaume na Waumini wanawake wao  
kwa wao ni marafiki  
walinzi...}(Tawba71)

Yaani baina ya waumini kuna mapenzi  
na kunusuriana na kusaidiana,na baina  
yao kuna kuzoweana baina ya  
waislam.

Na ushahidi nikaulia ya Mwenyezi Mungu: { Huwakuti watu wanao muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho kuwa wanawapenda wanao mpinga Mwenyezi Mungu na Mtume wake, hata wakiwa ni baba zao, au watoto wao, au ndugu zao, au jamaa zao. Hao ameandika katika nyoyo zao Imani, na amewapa nguvu kwa Roho itokayo kwake. Na atawaingiza katika Mabustani yapitayo mito kati yake. Humo watakaa daima. Mwenyezi Mungu awe radhi nao, na wao wawe radhi naye. Hao ndio Hizbullahi, Kundi la Mwenyezi Mungu. Hakika Kundi la Mwenyezi Mungu ndilo lenye kufanikiwa}.(AlMujaadalah 22)

Maneno hayo ameelezwa mtume  
(s.a.w) kwamba hayatokei hayo wala  
hayapo kamwe kwamba awe mtu  
nimwenye kumuamini Mwenyezi  
Mungu na mtume wake akawa  
anawapenda makafiri, ikiwa  
atawapenda basi huyo hawi nimuumini  
hatakama anadai kua yeye ni muumini.

Alisema ibn Qayyim Allah  
amrehemu:

Unawapenda maadui wa kipenzi na  
unadai Kumpenda!

Haiwezekani kupatikana mapenzi.

Kisha unawafanyia uadui nakuwapiga  
vita wapenzi wake!

## Yakowapi mapenzi ewe ndugu wa Shetani!

Hilo haliwezekani kamwe kuwapenda makafiri,**kasha anasema:mimi nampenda Mwenyezi Mungu na mtume wake (s.a.w) kwakauli yake Mwenyezi Mungu:** {Enyi mlio amini! Msiwafanye adui zangu na adui zenu kuwa marafiki mkiwapa mapenzi,...}(**Al Mumtah'inah1**) mpaka alipo sema **Mwenyezi Mungu:**

{**Hakika nyinyi mna mfano mzuri kwenu kwa Ibrahim na wale walio kuwa pamoja naye, walipo waambia watu wao:** Hakika sisi tumejitenga nanyi na hayo mnayo yaabudu badala ya **Mwenyezi Mungu.** Tunakukataeni;

na umekwisha dhihiri uadui na chuki baina yetu na nyinyi mpaka mtakapo muamini Mwenyezi Mungu peke yake...} (Al Mumtah'nah 4).

Na amesema Mwenyezi Mungu: {Wala haikuwa Ibrahim kumtakia msamaha baba yake ila kwa sababu wa ahadi aliyo fanya naye. Lakini ilipo mbainikia kwamba yeye ni adui ya Mwenyezi Mungu, alijiepusha naye. Hakika Ibrahim alikuwa mwingi wa kuomba, mnyenyekemu, mvumilivu} (Tawba 114).

Hii ndio dini ya nabii Ibrahim alimkana baba yake na ndie mtu wakaribu wakati alipo baini kua niaduwi wa Mwenyezi Mungu.

Na aya zimeonyesha pia kua  
kuwapenda makafiri kunapingana na  
imani ya kumuamini Mwenyezi  
Mungu nasiku ya Qiyama,ima katika  
asili ya imani au ukamilifu wake,lakini  
ikiwa kuwapenda kwao nipamoja na  
kuwaunga mkono katika midhehebu  
yao au mwenendo wao na ukafiri wao  
basi huko nikutoka katika uislam.

Na ama ikiwa nikuwapenda bila ya  
kuwanusuru hii inazingatiwa kua  
niyenye kupunguza imani,na niuovu  
ambao una dhofisha imani.

Na kauli ya Mwenyezi Mungu  
:{hao }inakusudia wale ambao wanao  
wanajitenga mbali na mapenzi ya  
kuwapenda wale wenye kumfanyia

uadui Mwenyezi Mungu na mtume wake.

Na maana ya kauli ya Mwenyezi Mungu: { Hao ameandika katika nyoyo zao Imani }

Yaani amethibitisha Mwenyezi Mungu katika nyoyo zao na akazamisha katika nyoyo zao imani.

Na ndio Mwenyezi Mungu akasema{na amewapa nguvu kwa Roho itokayo kwake. Na atawaingiza katika Mabustani yapitayo mito kati yake}.

Alisema Mwenyezi Mungu mtukufu{ Sema: Ameiteremsha hii Roho takatifu kutokana na Mola wako

Mlezi kwa haki, ili awathibitishe wale walio amini, na kuwa ni uwongofu, na ni bishara kwa Waislamu } (An Nahl102)

Na alisema Mwenyezi Mungu:

{ Ameuteremsha Roho muaminifu, }  
(Shu'araa193).

Na amewapa nguvu kwa Roho itokayo kwake,yaani aliwapa nguvu kutoka kwa Mwenyezi Mungu mtukufu,na nguvu ya imani katika dunia,na akhera atawaingiza peponi pepo ambayo ina miti ilio shikana na mito na majumba mazuri.

Na amesema Mwenyezi Mungu katika kuisifu pepo:{ Na atawaingiza katika

Mabustani yapitayo mito kati  
yake...}na wataishi humo bila  
kutolewa,alisema Mwenyezi Mungu  
mtukufu{ Watadumu humo;  
hawatataka kuondoka}{(kahf 108. )

Hawata ogopa kifo wala yoyote atakae  
kuja kuwatowa peponi,au kuwafukuza  
mfano wa yaliomo duniani,anaweza  
kua mtu duniani katika majumba  
mazuri lakini hawezi kusalimika na  
umauti ukamtowa katika majumba  
hayo,na pia hasalimiki na maadui  
kumvamia na kumtoa,mwanadamu  
daima katika dunia nimwenye  
kuogopa.

Kauli ya Mwenyezi  
Mungu:{Mwenyezi Mungu awe radhi

nao, na wao wawe radhi  
naye...} walipo wachukiza ndugu zao  
makafiri na wakawafanyia uadui  
aliwapa Mwenyezi Mungu ridhaa  
kutoka kwake Mwenyezi Mungu  
mtukufu malipo yao,hakika wao  
walipewa badala ya ya yale maudhi ya  
ndugu zao makafiri walipewa ridhaa  
ya Mwenyezi Mungu mtukufu  
aliwaridhia Mwenyezi Mungu na wao  
wakaridhika.

Kauli ya Mwenyezi Mungu{ hao ndio  
kundi la Mwenyezi Mungu }yaani ndio  
jamaa wa Mwenyezi Mungu ama  
makafiri nikundi la shetani amesema  
Mwenyezi Mungu { hao ndio kundi la  
shetani }(almujaadala 19) .

yaani ndio jamaa wa shetani na ndio  
wanao mnusuru shetani,

Na ama waumini ndio wanao mnusuru  
Mwenyezi Mungu mtukufu.

Maswala haya yana ambatanana  
kuwafanyia uadui makafiri na kuto  
kuwapenda,**na haipelekei kwamba**  
**tukate uhusiyano na makafiri katika**  
mambo yenye manufaa ya kidunia bali  
kuna mambo ambayo yanayo toka  
katika hukumu hii:

1.Pamoja na kuwachukia na  
kuwafanyia uadui niwajibu kwetu  
kuwalingania wamfuate Mwenyezi  
Mungu mtukufu,**niwajibu tuwalinganie**  
**waingie ndani ya uislam na tusiwaache**  
tukasema:

Hao nimaaduwi wa Mwenyezi Mungu na nimaadui zetu na inapaswa kwetu tuwalinganie wamfuate Mwenyezi Mungu huwenda Mwenyezi Mungu akawaongoza.

2.Hakuna pingamizi kufanya mkataba na makafiri ikiwa waislam watahitaji hilo,kwakuwa waislam hawawezi kuwapiga vita,na inahofiya kwa waislam shari zao.

3.Hakuna pingamizi kuwalipa kwa wema wao kwa waislam,hakuma kiziwizi kuwalipa kwa wema walio ufanya,**amesema Mwenyezi Mungu mtukufu:**

{ Mwenyezi Mungu hakukatazini kuwafanyia wema na uadilifu wale

ambao hawakukupigeni vita, wala hawakukutoeni makwenu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao uadilifu}.(Al Mumtah'nah 8).

4.Mzazi akiwa nikafiri inapasa kwa mtoto wake muislam amfanyie wema,**lakini asimtii katika ukafiri kwa kauli ya Mwenyezi Mungu mtukufu:**

{Na tumemuusia mtu kwa wazazi wake wawili. Mama yake ameichukua mimba yake kwa udhaifu juu ya udhaifu, na kumwachisha ziwa baada ya miaka miwili. (**Tumemuusia**): Nishukuru Mimi na wazazi wako. Ni kwangu Mimi ndiyo marudio(**14**).

Na pindi wakikushikilia kunishirikisha na ambayo huna ilimu nayo, basi usiwat'ii. Lakini kaa nao kwa wema duniani, nawe ishike njia ya anaye elekea kwangu. Kisha marejeo yenu ni kwangu Mimi, na Mimi nitakuambieni mliyo kuwa mkiyatenda }([Luqman14-15](#))

Mzazi ana haki akiwa kafiri, lakini usimpende mapenzi ya moyoni, bali unamfanyia wema kama ujira wa kukulea nakwasababu yeye nimzazi,na ana haki kwako umfanyie wema.

5.Kubadilishana biashara pamoja na makafiri na kununua kwao, na kununua mahitaji kwao na kuchukua bidhaa na silaha utoka kwa makafiri

kwa kulipia pesa hilo halina tatizo,na  
alikuwa Mtume (**s.a.w**) ana alifanya  
kazi na makafiri,na alifanya kazi  
mtume (**s.a.w**)na watu wa khaybar nao  
ni Mayahudi alifanya nao kazi ya  
walime shamba kwa makubaliyano ya  
kile kitakacho vunwa kutoka  
shambani,kufanya hivyo sio  
kuwapenda makafiri,bali  
nikubadilishana masilahi.

Niwajibu tufahamu mambo haya,na  
hayaingii katika kuwapenda makafiri  
na hayakukatazwa.

Hakuna makatazo ya haya kwasababu  
mambo hayo niyakidunia  
na maslahi hayana maana ya mapenzi  
moyoni,lazima tutofautishe baina ya

maslahi na kupenda,kwasababu kuna baadhi ya watu wakisikia dalili za kuwafanyia uaduwi makafiri na kuto kuwapenda huwenda wakafahamu kua hawafanyi nao kazi za kidunia,na hawafanyi mawasiliano na makafiri,na wanaelewa kua nikukata mafungamano nao moja kwa moja,

Hapana!kuwapenda makafiri na kuwafanyia uadui kumewekewa mipaka kwa hukumu na mipaka na masharti zinazo julikana kwa wana wachuoni ilio chukuliwa kutoka katika Quraan na sunna za mtume (**s.a.w**).

6.Mwenyezi Mungu Alihalalisha kuoa wanawake wa kiyahudi na kinaswara kwa sharti wawe niwenye kujihifadhi

na kujiweka mbali na zinaa katika  
heshima zao, na akahalalisha  
Mwenyezi Mungu kula wanyama  
walio chinjwa na mayahudi na  
manaswara.

7. Hakuna ubaya kuitikia wito wao na  
kula chakula cha halali kama alivyo  
fanya mtume (**s.a.w**).

8. Kuwafanya wema majirani ambao  
nimakafiri kwasababu wana haki ya  
ujirani.

9. **Haifai kuwadhulumu makafiri**  
**alisema Mwenyezi Mungu**  
mtukufu: { ... Wala kuchukiana na watu  
kusikupelekeeni kutofanya uadilifu.  
Fanyeni uadilifu. Hivyo ndio kuwa

karibu mno na uchamngu...} (Al-Maida8).

Fahamu Mwenyezi Mungu akuongoze kwa kumtii

Maneno haya nikama mwanzo wa ujumbe watatu kwasababu zimepita jumbe mbili:

-**Ujumbe wakwanza:** Nimaswala manne ambayo yalikusanya suratu Al Asri,

-**Ujumbe wapili:** Nimaswala ya matatu ambayo yamepita.

-**Ujumbe watatu:** Ndio hii,na utakuja ujumbe wa Nne nao una maswala ma Nne.

Kaanza mtunzi wa kitabu kwa kusema :**(Mwenyezi Mungu akuongoze)** hii ni dua ya shekh Allah amrehemu kwa kila atakae soma ujumbe huu kwa lengo la kuufahamu na kutafuta elimu kwa kusoma ujumbe huu,kwamba **Mwenyezi Mungu amuongoze,**

Na muongozo ni Mwenyezi Mungu kukuongoza kupita njia ya sawa na kukupa taufiiqi ya kupata elimu yenye manfaa,na kufanya matendo mema,na uongofu nikinyume cha upotovu,

Amesema Mwenyezi Mungu mtukufu: { **Kwani Uwongofu umekwisha pambanuka na upotofu**} (Al-Baqara 256)

Na amesema Mwenyezi Mungu mtukufu: {Na wao wakiona kila Ishara hawaiamini. Wakiiona njia ya uwongofu hawaishiki kuwa ndiyo njia; lakini wakiiona njia ya upotofu wanaishika kuwa ndiyo njia}.( Al-A'raaf)

Na uongofu katika aya makusudio yake nidini ya uislam,na upotovu unakusudiwa dini ya Abuu Jahli,(Allah amlani).

Hakika muislam pindi anapo ongozwa na Mwenyezi Mungu akawa nimenye kumtii basi atakuwa nimwenye kufanikiwa katika duniani na akhera,na kutii nikutekeleza maamrisho ya Mwenyezi Mungu nakujiepusha

makatazo yake,huko ndio kumtii  
Mwenyezi Mungu,

Mwanadamu anatakiwa umtii  
Mwenyezi Mungu katika maamrsho  
yake uyafanye,na katika makatazo  
yake ujiepushe kuyafanya  
kwakutekeleza amri za Mwenyezi  
Mungu,na kutarajia malipo yake  
Mwenyezi Mungu mshindi mtukufu na  
utarajie thawabu zake,na uogope  
adhabu zake,yoyote atakae pewa  
taufiiqi ya kumtii Mwenyezi Munguna  
akaongozwa kuwa nimwenye umtii  
Mwenyezi Mungu hakika atakuwa  
nimwenye mafanikio duniani na  
akhera.

## **UJUMBE WA TATU UISLAM NDIO DINI YA NABII IBRAHIM.**

Nini maana ya Uhanaifiyyah:

Uhanaifiya ambao muislam anatakiwa ajifundishe na aujue nikwamab uhanaifiyyah:Nidini ambayo alikuwa nayo Nabii Ibrahim (s.a.w).

Nayo nidini ambayo inapingana na ushirikina na inaanirisha wanadamu woote washikamane na Tauhiid(**kumpwekesha Mwenyezi Mungu mmoja bila kumshirikisha na chochote**).

Na nabii Ibrahim (s.a.w) alikuwa mwenye Uhanaifiyyah na ni Muislam,

Uhanafiya wa nabii Ibrahimu maana yake alikuwa nimwenye kupinga ushirikina, na nimwenye kumpwekesha Mwenyezi Mungu(**Tauhidi**),na nimwenye kufanya ibada zake zoote kwajili ya Mwenyezi Mungu,**alisema Mwenyezi Mungu mtukufu:**{. Hakika Ibrahim alikuwa mfano mwema, mnyenyekemu kwa MwenyeziMungu, mwongofu, wala hakuwa mionganini mwa washirikina}(**An Nahl 120**).

Uhanafiyyah nikatika sifa za nabii Ibrahim (**s.a.w**) ambayo maana yake nikupuuziya na kupiga vita ushirikina na nimwenye kuelekea moja kwamoja kwenye Tauhidi.

Alielekea kwenye Tauhidi katika mambo yake yote nakuwa na ikhlasi katika mambo yake yote,**amesema MwenyeziMungu mtukufu:**{ Kisha tukakufunulia ya kwamba ufuate mila ya Ibrahim, mwongofu,wala hakuwa miongoni mwa washirikina}(**An Nahl 123**).

Na amesema **Mwenyezi Mungu mrukufu:**

{ Ibrahim hakuwa Yahudi wala Mkristo, lakini alikuwa mwongofu Muislamu, wala hakuwa katika washirikina }

(**Al 'Imran67**)

Hizi nisifa kubwa za nabii Ibrahim(s.a.w) ambazo miongoni mwazo ni Alhanafiyyah nakwamba dini yake ni Alhanafiya nayo nidini ilio takasika kwaajili ya Mwenyezi Mungu mshindi mwenye nguvu,dini ambayo haina ushirikina ndani yake,na ameamrisha Mwenyezi Mungu Mtukufu mtume wake Muhammad (s.a.w)aifate dini ya nabii Ibrahim kwa kusema:{ Kisha tukakufunulia ya kwamba ufuate mila ya Ibrahim, mwongofu,wala hakuwa miongoni mwa washirikina }.(An Nahl 123.)

Na tukaamrishwa pia tufuate dini ya nabii Ibrahim (s.a.w)  
kwakusema:{ Yeye amekuteueni. Wala hakuweka juu yenu mambo mazito

katika Dini. Nayo ni mila ya baba yenu Ibrahim. Yeye (**Mwenyezi Mungu**) alikuiteni Waislamu }(**Hajj78**).

Nayo ndio dini ya mitume wote.

Lakini kwakuwa nabii Ibrahim (**s.a.w**) nimbora wa mitume baada ya Muhammad(**s.a.w**)alikutana katika njia ya kulingania kwenye Tauhiidi(**kumpwekesha Mwenyezi Mungu peke yake bila kumshirikisha na chochote**) na adhabu na mitihani ambayo hakuna mtume alie kutana nayo akasubiri,

Nakwakua nabii Ibrahim(**s.a.w**) ndio baba wa mitume,hakika mitume walio kuja baada yake woote nikatika kizazi chake(**s.a.w**) basi uislam ndio dini ya

mitume wote,na uislam(**Alhanafiyyah**)  
nikulingania watu wampwekeshe  
Mwenyezi Mungu mmoja na  
wasimshirikishe na chochote,hii ndio  
dini ya manabii wote,lakini zama ilipo  
kua kwa nabii Ibrahim msimamo kwa  
dini hii basi alinasibishwa kwake na  
mitume walio kuja baada yake,na  
mitume wote baada yake

Walikuwa kwenye dini ya nabii  
Ibrahim,nayo nidini ya kumpwekesha  
Mwenyezi Mungu mmoja bila  
kumshirikisha na chochote na  
kumtakasia utii Mwenyezi Mungu  
mtukufu(**yaani ibada zako zote ziwe**  
**kwa ajili ya Mwenyezi Mungu**).

Niipi dini hii ambayo ameamrishwa mtume Muhamad (s.a.w)kuifuata na tume amrishwa na sisi uifuata?

Niwajibu juu yetu kuijiwa,kwasababu muislam niwajibu kwake kuyajuwa yale aliyo muamrisha Mwenyezi Mungu ili kuyatekeleza,na haitoshi kujinasibisha na uislam bila kuufahamu uislam wake,na hajuwi mambo ambayo yanatengua uislam,na nizipi sheria za uislam, na hukumu za uislam, na haitoshi kujinasibisha na dini ya nabii Ibrahim(s.a.w) ilihali hauijuwi,na utakapo ulizwa kuhusu dini ya nabii Ibrahim(s.a.w) unasema: sijuwi, kuwa hivyo kwa muislam haifai, niwajibu uijuwe dini yako

vizuri ili uifuate ukiwa unaijuwa na ili usiache chochote ila umekitekeleza.

**NIWAJIBU KWA MWANADAMU  
AMUABUDU MWENYEZI MUNGU  
PEKE YAKE NA AFANYE IBADA  
ZOTE KWAAJILI YA MWENYEZI  
MUNGU.**

Dini ya nabii  
Ibrahim(**s.a.w**),inafundisha kumuabudu  
Mwenyezi Mungu mmoja na kufanya  
ibada zote kwa ajili ya Mwenyezi  
Mungu,nakumtakasia dini.

Kufanya hivyo kunatakiwa mambo  
mawili:

1.Kufanya Ibada.

## 2.Kuwa na Ikhlasi (**kufanya ibada zote kwa ajili ya Mwenyezi Mungu**).

Atakae muabudu Mwenyezi Mungu na hakuwa na ikhlasi haitakuwa amefanya ibada yoyote, mwenye kumuabudu Mwenyezi Mungu ,akafunga na akahiji,na akaswali au kufanya umra,na akatoa sadaka,na akatoa zaka,na akafanya ibada nyingi lakini hakuzifanya kwa ajili ya Mwenyezi Mungu mtukufu katika ibada zake,ima kwasababu ya kujionyesha(**Riyaa**) au kwa kutaka sifa,au amechanganya ibada yake na chochote katika mambo ya ushirikina,kama kuomba kisichokua Mwenyezi Mungu,au kuomba nusra kwa asie kua Mwenyezi Mungu,au kuchinja kwa asie kua Mwenyezi

Mungu,hakika mtu wa namna hiyo hatakuwa amefanya ibada kwa ajili ya Mwenyezi Mungu,bali atakuwa ni Mshirikina,na hatakuwa katika dini ya nabii Ibrahim(s.a.w).

Wengi mionganini mwa wanao jinasibisha kwenye uislam katika zama zetu wana angukia katika shirki kubwa kwa sababu ya kuomba asie kuwa Mwenyezi Mungu,nakuabudu makaburi nakuchinja kwenye makaburi,na kuyatolea nadhiri makaburi,na kutufu kwenye makaburi na kutabaruku (**kutaka baraka**) kwenye makaburi,nakuomba nusra kwa watu waio kufa namengineyo,nawao wanasema niwaislam.

Hao hawakujuwa dini yao au  
waliijuwa wakapinga wakiwa  
wanajuwa na hali hii ndio mbaya zaidi  
Mwenyezi Mungu atukinge.

Dini ya nabii Ibrahim (**s.a.w**) haikubali  
ushirikina kwa namna yoyote itakavyo  
kuwa na atakae changanya ibada yake  
na ushirikina basi hatakuwa katika dini  
ya nabii Ibrahim (**s.a.w**),hatakama  
atajinasibisha na dini hiyo,na akadai  
kuwa ni muislam,jambo la wajibu  
nikuijua dini ya nabii Ibrahim (**s.a.w**)  
na kuifanyia kazi na ujilazimishe nayo  
kwa kumuabudu Mwenyezi Mungu  
peke yake na kumtakasia ibada bila ya  
kumshirikisha.

Isiwe katika ibada zako chochote  
katika ushirikina sawa ikiwa nishirki  
ndogo au shirki kubwa.

Hii ndio dini ya nabii I brahim (**s.a.w**)  
ilio takasika na shirki na kuupiga vita  
ushirikina kwa aina zake zote na  
ikahimiza watu washikamane na  
Tauhiidi kwa ujumla wake nakuwataka  
watu wote wamuabudu **Mwenyezi**  
**Mungu** mmoja na kumtakasia ibada.

Na kwasababu hiyo ameamrisha  
**Mwenyezi Mungu** watu wote na  
aliwaumba kwasababu ya ibada.

Katia maneno kuna ishara ya kua  
mwanadamu anatakiwa amuabudu  
**Mwenyezi Mungu** kwa kumtakasia  
dini,yani afanye ibada kwa ajili ya

Mwenyezi Mungu,ameamrisha  
Mwenyezi Mungu watu  
wote,kawaamrisha watu wajinsia zote  
,watu wote tangu kwa Adamu mpaka  
kwa binadamu wamwisho katika dunia  
hii,wote Mwenyezi Mungu kawa  
amrisha Mwenyezi Mungu  
wamuabudu yeye na wamtakasie  
ibada, **anasema Mwenyezi Mungu**  
**mtukufu:**{ Enyi watu! muabuduni  
Mola wenu mlezi aliye kuumbeni  
nyinyi na wale wa kabla yenu, ili  
mpate kuokoka}.

Mwenyezi Mungu) ambaye  
amekufanyieni hii ardhi kuwa kama  
tandiko, na mbingu kama paa, na  
akateremsha maji kutoka mbinguni, na  
kwayo akatoa matunda yawe riziki

zenu. Basi msimfanyizie Mwenyezi Mungu washirika, na hali nyinyi mnajua}.(Al Baqaraa21-22)

Hakika Mwenyezi Mungu hana mfano,na hana anae fanana nae, wala wala anae lingana nae, nahaya nimakatazo ya shirki kubwa na shirki ndogo.

Ameamrishaa Mwenyezi Mungu watu wote wakwanza wao na wamwisho wao.

Na Mwenyezi Mungu kawaumba kwasababu ya ibada wamuabudu yeye peke yake bila kumshirikisha, na wanadamu wameumbwa kwasababu ya ibada,**kama alivyo sema Mwenyezi Mungu :{Nasikuumba majini wala**

watu ila kwasababu waniabudu } (Al dhariyati 56).

na wameamrishwa hivyo katika k kauli yake Mwenyezi Mungu mtukufu: { Enyi watu mlion amini muabuduni mola wenu ambae ale kuuumbeni } (Al Baqara 21).

Hii ndio maana ya kusema  
(Kakuumbeni Mwenyezi Mungu  
kwasababu ya ibada na akawaamrisha  
waitekeleze ibada),

Imekusanya kauli hii mambo mawili:

1. Mwenyezi Mungu amewamrisha waja wake wafanye ibada.
2. Mwenyezi Mungu amewaumba waja wake kwasababu ya ibada,

Kama alivyo sema Mwenyezi mungu: {Sikuwaumba majini na wanadamu ila waniabudu} kauli ya Mwenyezi mungu {sikuwaumba majini na watu} Mwenyezi mungu ndie muumbaji yeye ndie alie umba vitu vyote na kayika hivyo aliumba majini na watu na akawapa akili na akawalazimisha wamuabudu yeye peke yake wasimshirikishe na lolote na akatowa amri maalumu kwa majini na watu wamuabudu yeye Mwenyezi mungu peke yake,kwasababu Mwenyezi mungu amewapa akili na akawapa maarifa yakupambanua kitu chenya madhara na chenye manufaa,na ja jambo lahaki na labatili,na akaumba mambo mengi kwa maslahi ya majini na watu na manufaa yao.

anasema Mwenyezi mungu:{ Na amefanya vikutumikieni vilivyomo mbinguni na vilivyomo katika ardhi, vyote vimetoka kwake. Hakika katika hayo zimo Ishara kwa watu wanao fikiri }(Al jathiya 13)

Vyote vimewekwa kwa ajili ya mwanadamu ili avitumie kuweza kufikia lengo la kuletwa hapa duniani ambalo ni Ibada.

Anasema Mwenyezi mungu {Sikuwaumba majini wala watu ila waniabudu}.

Majini niulimwengu usio onekana hatuwaoni majini,na majini wamelazimishwa kufanya ibada,na wamekatazwa kufanya shirki na maasi

kama mwanadamu,ispokua majini  
wametofautiyana na wanadamu katika  
maumbile.

Ama upande wa maamrisho na  
makatazo majini nikama bianadamu  
hakuna tofauti wao wameamrishwa na  
wamekatazwa,majini hawaonekani na  
hatuwezi kuwaona ila

wapo na watu ndio watoto wa  
Adamu(**s.a.w**)wanadamu wanasifa ya  
kufurahishana na wanaishi pamoja hii  
ndio sababu ya kuitwa binadamu kua  
**(Watu)**.

Ama majini wameitwa majini  
kwasababu wamejificha na hatuwezi  
kuwaona,

Majini wamefichwa kwa wanadamu na  
hatuwezi kuwaona.

Ulimwengu wa majini upon a mwenye  
kukanusha kuto kuwepo majini basi  
atakuwa amekufuru,kwasababu  
atakuwa amemkadhibisha Mwenyezi  
mungu na mtume wake (**s.a.w**) na  
makubaliano ya wanachuoni,hakika  
amebainisha Mwenyezi mungu  
mwenye nguvu kwamba yeye  
hakuumba majini na watu ispokuwa  
kawaumba kwa ajili ya Ibada na sio  
kwasababu nyingine.

Mwenyezi mungu hakuwaumba majini  
na watu ili wamnufaishe au  
wamdhuru,au ajitukuze kwasababu ya  
kuwaumba kutokana na udhaifu,au

ajione yuko na watu au majini wengi  
hayko mpweke,kwasababu Mwenyezi  
anajitoshelezea na walimwengu,na  
hakuwaumba kwasababu  
anawahitajia,hakuwaumba ili  
wamruzuku au wamtafutie mali,**bali**

**Mwenyezi mungu anasema  
kuyakanusha yote hayo :{Na sitaki  
kwao riziki, wala sitaki wanilishe (57)  
Hakika Mwenyezi Mungu ndiye  
Mwenye kuruzuku, Mwenye nguvu,  
Madhubuti } (Dhaariyaat 57-58).**

Mwenyezi mungu hana haja na  
viumbe,ispokuwa aliwaumba majini na  
wanadaamu kwa kitu kimoja nacho ni  
ibada, Mwenyezi mungu hana haja ya  
ibada zao bali wao ndio wanao

hzihitajia ibada zao,kwasababu  
watakapo muabudu Mwenyezi mungu

Atawakirimu na atawaingiza  
peponi,basi maslahi ya Ibada  
yanawarudia wanadamu wenyewe,na

madhara ya maasi yanawarudia  
wenyewe,ama Mwenyezi mungu alie  
tukuka na wajuu hakumdhuru kutii  
kwa mwenye kumtii wala maasi ya  
mwenye kumuasi,**alisema Mwenyezi  
mungu :{Na Musa alisema: Mkikufuru  
nyinyi na wote waliomo duniani,  
hakika Mwenyezi Mungu ni Mkwasi,  
Anajitosha, Msifiwa}(Ibrahim 8)**

Mwenyezi mungu hayamdhuru maasi  
ya mwenye kumuasi wala  
hakumnufaishi kutii kwa mwenye

kumtii ispokua ibada na maasi  
yanarudi kwa nafsi zao wenyewe,pindi  
watakapo mtii Mwenyezi mungu  
watanufaika na wakimuasi Mwenyezi  
Mungu watadhurika kwa kumuasi  
Mwenyezi Mungu.

**NA MAANA YA QAULI YA**  
**MWENYEZIMUNGU {ILI**  
**WANIABUDU}.**

Maana yake ili wampwekeshe  
Mwenyezi mungu na wamfanye  
Mwenyezi mungu kuwa nimmoja  
pekeyake katika ibada,

Na katika maneno hayo kuna majibu  
kwawale wanao sema kua Tuhiidi:  
Nikukiri kuwa Mwenyezi mungu  
nindie muumbaji na nimwenye kutowa

rizki na ndie mwenye kuhuyisha na nimwenye kufisha,na ndie mwenye kupangilia mipango yote ya duniani,hii nitauhidi lakini sio tauhidi ambayo kwasababu yake aliumba Mwenyezi mungu viumbe ,ispokua aliumbwa viumbe kwasababu ya kumpwekesha Mwenyezi mungu katika kumfanyia ibada.

Ama mwenye kukiri kuwa Mwenyezi mungu ndio mwenye kuumba na kutoa rizki imani hiyo haitoshi kua nimwenye tauhidi na hawezi kuingia peponi kwa imani hiyo,bali atakuwa katika watu wa motoni kwasababu hakuleta tauhidi ambayo ndio sababu ya kuumbwa kwake ambayo ni Kumpwekesha Mwenyezi mungu

katika utekelezaji wa ibada  
nakuzifanya ibada zote ziwe kwa ajili  
ya Mwenyezi mungu.

**JAMBO KUBWA ALILO**  
**AMRISHA MWENYEZI MUNGU**  
**WAJA WAKE NI TAUHIIDI.**

Hakika tauhiid ndio jambo kubwa alilo  
amrisha Mwenyezi mungu sheria zote  
za Mwenyezi mungu zilikuja baada ya  
tauhiid.

Na ushahidi wa hilo nikauli ya  
Mwenyezi mungu mtukufu  
idemayo: { Muabuduni Mwenyezi  
Mungu wala msimshirikishe na  
chochote. Na wafanyieni wema wazazi  
wawili na jamaa na mayatima na  
masikini na jirani wa karibu na jirani

wa mbali, na rafiki wa ubavuni na  
mpita njia, na walio milikiwa na  
mikono yenu ya kulia. Hakika  
Mwenyezi Mungu hawapendi wenye  
kiburi wanao jifakhiri, } (Al-Nnisaa 36)

Aya hii ndani yake kuna haki  
kumi(10),**kwasababu hiyo inaitwa aya  
hiyo :** (Ayya yenyе haki kumi).

Haki hizo kumi yakwanza nihaki ya  
Mwenyezi mungu mtukufu ambayo  
nikumuabudu Mwenyezi mungu  
pekeyake bila kumshirikisha na  
chochote, nakuwafanyia wema wazazi  
wawili, nakuwafanyia wema jamaa  
wakaribu,na mayatima nk.

Jambo lamuhimu nikwamba  
Mwenyezi mungu katika hizo haki

kaanza kwakutaja haki yake pale alipo sema : { na msimshirikishe na lolote } hakutosheka nakusema :{ Muabuduni **Mwenyezi mungu** },kwasababu ibada haiswihi ikiwa na shirki ndani yake na haina manufaa yoyote,na haiitwi ibada mpaka itakapo kuwa nikwaajili ya **Mwenyezi mungu** peke yake na ikiwa pamoja na shirki basi haiwi ni ibada kwavyovyote atakavyo mata shida na taabu katika kuifanya hiyo ibada, amekutanisha amrri ya kumuabudu **Mwenyezi mungu** pamoja na amri ya kujiepusha na shirki kuonyesha kuwa haiswihi ibada yoyote ikiwa na shirki ndani yake.

Hii nidalili kuwa jambo kubwa alilo amrisha **Mwenyezi mungu** ni

tauhiid(Kumpwekesha Mwenyezi mungu katika ibada) kwasababu Mwenyezi mungu kaanza kuizungumzia katika aya nyingi ikiwemo ayay ilio pita,**na katika ayah ii :{Na Mola wako Mlezi ameamrisha kuwa msimuabudu yejote ila Yeye tu }** (Israa23).

Akaanza Mwenyezi mungu kuizungumzia tauhiid,nah ii inaonyesha kuwa tauhiid ndio jambo kubwa alilo amrisha Mwenyezi mungu.

Amesema Mwenyezi mungu mtukufu:{ Sema: Njooni nikusomeeni aliyo kuharimishieni Mola wenu Mlezi. Nayo ni kuwa, msimshirikishe

Yeye na chochote. Na wazazi wenu wafanyieni wema. Wala msiwauwe watoto wenu kwa sababu ya umasikini.

Sisi tunakuruzukuni nyinyi na wao.

Wala msikaribie mambo machafu, yanayo onekana, na yanayo fichikana. Wala msiuwe nafsi ambayo Mwenyezi

Mungu ameharimisha kuiuwa, ila ikiwa kwa haki. Hayo amekuusieni ili myatie akilini } (Al Anaam 151).

Hii ni dalili ya mambo yanayokuja ya kwamba jambo kubwa aliloliikataza Allah ni shirki, basi itakapokua jambo kubwa aliloliamrisha ni tauheed, niwajibu kwa mwanadam aanze kuisoma aqidah kabla ya kitu chochote, aqidah ndio msingi, basi ni wajibu kwa mwanadam aanze kuisoma

na kuifundisha, na adum katika  
kuifundisha na kuibainisha kwa watu,  
kwa sababu ndio jambo kubwa  
aliloliamrisha Allah, siyo munasaba  
kulifanya liwe jambo la mwisho au  
lipewe umuhimu, kwasababu kuna  
walinganiaji wanaacha kuifundisha  
tauheed na aqidah, watu wamepewa  
mtihani katika jambo hili.

Na kwasababu kulipuuzia jambo hili  
nikuipuuzia dini basi niwajibu kulipa  
kipao mbele.

## **NINI MAANA YA TAUHIDI?**

Je Tauhiid nikukiri kuwa Mwenyezi  
mungu nimuumba na nimtoa rizki na  
ndie anaefisha na kuhuyisha?

La , Tauhiid nikumpwekesha  
Mwenyezi mungu kwakufanya  
ibada,**kwasababu Mwenyezi mungu**  
**alisema:**{ Sikuumba majini wala watu  
ila waniabudu }(Dhariyat 56).

Walisema wanawachuoni wa tafsiri :  
maana ya neon (**Ili waniabudu**):maana  
yake wanipwekeshe, walitafsiri neno  
Tauhiid kwamaana ya Ibada.

Ikiwa nihivyo Maana ya Tauhiid  
;Nikumpwekesha Mwenyezi mungu  
kwakufanya ibada,na sio kukiri  
kuwa Mwenyezi mungu ndie  
muumbaji na mtowa rizki na mwenye  
kuhuyisha na kufisha na kupangilia  
mipango yoote ya ulimwengu,

kwasababu hayo yanajulikana  
kimaumbile,na yapo akilini ,hakuna  
yoyote mwenye akili asie juwa kuwa  
Mwenyezi mungu alie umba mbingu  
na ardhi kuwa ni Mwenyezi mungu,  
nahakuna yoyote duniani akiwemo  
kafiri na mwenye kupinga kuwepo  
kwa Mwenyezi mungu anae amini  
kuwa kuna binaadamu alie umba  
mwanadamu mwanadamu mwenzake,  
**alisema Mwenyezi mungu**  
**mtukufu:** {Na pindi utakapo wauliza  
nani alie waumba wanasema ni  
Mwenyezi mungu} (Al Zukhruf 87)  
hakuna yoyote mwenye akili duniani  
ane amini kuwa mwanadamu  
anaweza kumuumba mwanadamu  
mwenzake kasha akatembea na akala  
chakula na kuzuzungumza je yupo

yoyote ambae anae weza kufanya  
hivyo?

Mwenyezi mungu mtukufu anasema :

{ Au wao wameumbwa pasipo  
kutokana na kitu chochote, au ni wao  
ndio waumbaji? ( 36). Au wao  
wameziumba mbingu na ardhi? Bali  
hawana na yakini. } (Al Tuur 35-36).

Tauhid ya kumpwekesha Mwenyezi  
mungu kwa matendo ya Mwenyezi  
mungu kama kuumba nk ipo katika  
maumbile ya mwanadamu na katika  
akili za wanadamu, lakini haitoshi bila  
mwanadamu kumpwekesha Mwenyezi  
mungu katika kufanya ibada nako  
nikufanya ibada kwa ajili ya  
Mwenyezi mungu.

Tauhid nikumpwekesha Mwenyezi  
Mungu ,na sio kumpwekesha  
Mwenyezi Mungu kwa kuumba kwake  
na kutowa rizki na kuhuyisha na  
kufisha ,kwasababu mambo hayo  
yanajulikana ,na haitoshi tauhid ya  
vitendo vyta Mwenyezi Mungu katika  
kuitambulisha tauhidi.

TNB: Ndugu katika imani hii  
nisehemu ya tatu katika kitabu hiki cha  
Masomo katika umuhimu wa Tawhid .  
Muhtasari wa kitabu cha Al-Usulu AL-  
Thalathah cha Imamu Fawzani Allah  
amuhifadhi tuwe pamoja katika  
sehemu ya nne ijayo Allah akiipenda .

### **Utangulizi:**

Kaanza kwa kusema Bismi llahi  
Rrahmani Rrahim; Kwajina la  
Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma  
mwenye kurehemu.

Ameanza Mwenyezi Mungu  
Amrehemu risala hii kwa jina la  
Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma  
mwenye kurehemu, kwa kufuata  
kitabu cha Mwenyezi Mungu mshindi  
na mtukufu, kwa sababu macho yako  
yakiangalia ndani ya msahafu na kabla  
ya kila sura kuna (**Bismi llahi**  
**Rrahmani Rrahim**).

Kuanzia neno hili katika risala na  
katika vitabu nikufuata kitabu cha  
Mwenyezi Mungu mshindi na  
mtukufu, vilevile nabii Muhammad

(s.a.w) Alikua -ana mwambia muandishi- a'ndike mwanzo wa kila barua wakati anapo watumia viongozi na maraisi na waliyoko mbali ana walingania katika Uislamu, **anaanza kuandika:**

Kwajina la Mwenyezi Mungu  
Mwingi wa rehma mwenye kurehemu.

Na alikua Mtume (s.a.w) anaanza mazungumzo yake na maneno yake kwa: Bismi llahi Rrahmani Rrahim, yaonyesha kuanza kwa Bismi llahi Rrahmani Rrahim ni sunna ya Mtume (s.a.w), vilevile Nabii Sulaiman (s.a.w) alipo muandikia Malkia -Mfalme wa saba' Yemen- **ameanza kuandika kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa**

**rehma mwenye kuruhemu:** (Malkia akasema: Enyi wahishimiwa! Hakika nimeletewa barua tukufu\* Imetoka kwa Sulaiman nayo ni.

Kwajina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehma Mwenye kurehemu\* Msinifanyie jeuri, na fikeni kwangu nanyi mmekwisha kuwa wenyewe kusalimu amri).

(**An-Naml: 29-31**).

Inatakiwa kuanza na jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehma Mwenye kurehemu, katika kila jambo lenye umuhimu, na katika kila kitabu chenye umuhimu na thamani, na katika kila risala.

Kwa sababu hii wale ambao hawaanza kwenye vitabu vyao na risala zao kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehma Mwenye kurehemu, hao wameacha sunna ya Mtume na kuto kufuata kitabu cha Mwenyezi Mungu Mshindi na mtukufu, huenda kwa sababu hiyo vitabu vyao na risala zao hazina baraka na ndani yake hakuna faida; kwa sababu ikiwa hakuna jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehma Mwenye kurehemu huondolewa faida.

Risala ya kwanza Maswala manne ambayo yameambatana na Surati Al-Asr.

**Jambo kubwa alilo liataza**  
**Mwenyezi Mungu ni Shirki.**

na nijambo kubwa alilokataza  
Mwenyezi Mungu, [anasema](#): Ni Riba,  
ndio jambo kubwa alilokataza  
Mwenyezi Mungu, Uzinifu ndio jambo  
kubwa alilo kataza Mwenyezi  
Mungu,kwasababu hiyo wanatilia  
mkazo kukataza Riba na Uzinifu na  
tabia mbovu, lakini hawatilii  
umuhimu jambo la ushirikina na  
hawatahadharishi watu na  
ushirikina,haliyakuwa wanaona watu  
wameangukia katika ushirikina,huu  
niujinga mkubwa wakuto kujua sheria  
ya Mwenyezi Mungu mtukufu.

Jambo kubwa alilo kataza Mwenyezi  
Mungu niushirikina,nijambo kubwa  
kuliko ribaa na kunywa pombe,  
kuibana kula mali zawatu kwa batili,na

nikubwa kuliko kamari, shirki  
nidhambi kubwa kuliko dhambi  
yejote, **anasema Mwenyezi Mungu  
mtukufu:** {Sema: Njooni nikusomeeni  
aliyo kuharimishieni Mola wenu  
Mlezi, Nay o ni kuwa, msimshirikishe  
Yeye na chochote. Na wazazi wenu  
wafanyieni wema. Wala msiwauwe  
watoto wenu kwa sababu ya umasikini.  
Sisi tunakuruzukuni ninyi na wao,  
Wala msikaribie mambo machafu,  
yanayo onekana, na yanayo fichikana.  
Wala msiuwe nafsi ambayo Mwenyezi  
Mungu ameharamisha kuiuwa, ila  
ikiwa kwa haki. Hayo amekuusieni ili  
muyatie akilini **(151)** Wala  
msiyakaribie mali ya yatima ila kwa  
njia ya wema kabisa, mpaka afikie utu  
uzima. Na timizeni vipimo na mizani

kwa uadilifu. Sisi hatumkalifishi mtu ila kwa kadiri ya uwezo wake. Na msemapo semeni kwa uadilifu ingawa ni jamaa. Na ahadi ya Mwenyezi Mungu itekelezeni. Hayo amekuusieni ili mpate kukumbuka } (**Anaam 151-152**) .

Na Aya hizi zinaitwa: (**Nasaha kumi**).

Haya mambo yaharamu kaanza kuyazungumzia kwa kuanza na Shirki ikaonyesha kua ushirikina nidhambi kubwa aliyo ikataza Mwenyezi Mungu.

Na amesema Mwenyezi Mungu katika Aya nyingine: { Usimfanye mungu mwengine pamoja na Mwenyezi Mungu, usije ukawa wa kulaumiwa

uliye tupika} (Al Israa 22). Ameanza kukataza ushirikina na akamalizia kwa kukataza ushirikina kwa kusema :{ Haya ni katika hikima alizo kufunulia Mola wako Mlezi. Wala usimweke pamoja na Mwenyezi Mungu mungu mwengine, usije ukatupwa katika Jahannamu ukilaumiwa na kufurushwa} ( Al Israa 39), ikaonyesha kua jambo kubwa alilo likataza Mwenyezi Mungu ni ushirikina.

Na katika hadithi sahihi kutoka kwa Abdillah Bin Masuudi (s.a) hakika Mtume (s.a.w) aliulizwa: nidhambi gani kubwa? Akasema Mtume (s.a.w): ((Nikumfanya Mwenyezi Mungu kuwa na msaidizi nayeye ndiye aliye

kuumba)) kisha akaulizwa: kisha nini ?: akasema Mtume (s.a.w): ((Ni kumuua mtoto wako kwakuogopa asile na wewe)) kisha akaulizwa: kisha nini?: akasema Mtume (s.a.w) :((Nikuzini na binti wa jirani yako)) Imepokelewa na Bukhari (6861) na Muslim (86).

Akateremsha Mwenyezi Mungu kusadikisha hayo katika Kauli yake:{ Na wale wasio mwomba mungu mwengine pamoja na Mwenyezi Mungu, wala hawaui nafsi aliyo iharamisha Mwenyezi Mungu isipo kuwa kwa haki, wala hawazini - na atakaye fanya hayo atapata madhara } (Al furuqan-68) akaanza Mwenyezi Mungu kukataza Shirki.

Katika kauli ya Mtume (s.a.w):

"Nikumfanya Mwenyezi Mungu kuwa na msaidizi ilihali amekuumba" hii ni ishara ya kua Shirki nidhambi kubwa, kwasababu aliulizwa Mtume (s.a.w): Ni ipi dhambi kubwa? Akajibu kwa kuanza na shirki.

Kutoka kwa Abuu Hurayra (رض) hakika Mtume (s.a.w) Alisema: ((Jiepusheni na Madhambi saba yenyekuangamiza)) Akaulizwa: Niyapi hayo madhambi ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu?! Akasema:((Nikumshirikisha Mwenyezi Mungu, na uchawi, na kuuwa nafsi ambayo aliyo iharamisha Mwenyezi Mungu isiuliwe ila kwa haki)) Imetolewa na Bukhary (2766) na Muslim(89) .

Alianza Mmtume (s.a.w) kuelezea  
hayo madhambi yenyе kuangamiza  
kwa kuitaja shirki ikiwa ni dalili tosha  
kua shirki nidhambi kubwa,kwasababu  
hiyo hakika mwenye kufanya shirki  
haingii peponi milele,**Alisema**  
**Mwenyezi Mungu mtukufu:**{ Kwani  
anaye mshirikisha Mwenyezi Mungu,  
hakika Mwenyezi Mungu  
atamharamishia Pepo, na mahala pake  
ni Motoni. Na walio dhulumu  
hawatakuwa na wa kuwanusuru }(**Al  
Maida 72**)

**Mwenye kufanya Shirki**  
hatosamehewa na Mwenyezi Mungu,  
**alisema Mwenyezi Mungu**  
**mtukufu:**{ Hakika Mwenyezi Mungu  
hasamehe kushirikishwa, na husamehe

yaliyo duni ya hilo kwa amtakaye. Na anaye mshirikisha Mwenyezi Mungu basi hakika amezua dhambi kubwa. }

(Al Nnisaa 48).

Aya hizi zimeonyesha uharamu wa kuingia peponi kwa Mwenye kufanya shirki, na hakika Mwenyezi Mungu hatomsamehe mwenye kufanya Ushirikina, na ikaonyesha kuwa ushirikina nidhambi kubwa,kwasababu madhambi yasio kuwa Shiriki yanaseheka.

Anasema Mwenyezi Mungu mtukufu: { Hakika Mwenyezi Mungu hasamehe kushirikishwa, na husamehe yaliyo duni ya hilo kwa amtakaye }, hakika zinaa na wizi na kunywa pombe

na kula ribaa, atakaekufa bila kutubia  
atakuwa chini ya utashi wa Mwenyezi  
Mungu,akipenda atamsamehe na  
akipenda atamuadhibu.

Ama ushirikina hakika hausameheki,  
alihukumu Mwenyezi Mungu kwamba  
ye ye hamsamehemshirikina akifa  
kabla hajatubia, vile vile mwenye  
kufanya maasi hatakama anamadhambi  
makubwa yaliyo duni na shirki hakika  
madhambi hayo hayamfanyi pepo iwe  
haramu kwake,ima Mwenyezi Mungu  
amsamehe awe wakwanza kuingia  
peponi, ima amuingize motoni kisha  
atamtoa motoni baada ya kumuadhibu  
na amuingize peponi, Muumini  
vyovyyote atakavyo kuwa na uovu na  
maasi ambayo yako chini ya shirki

hakika hapaswi kukata tamaa na rehma ya Mwenyezi Mungu, na pepo haiwi ni haramu kwake, nayeye atakuwa chini ya msamaha wa Mwenyezi Mungu kwa utashi wake Mwenyezi Mungu mtukufu.

Ama mshirikina hakika yeye amenyimwa hayo yote - Mwenyezi Mungu atukinge na shirki-yote hayo yanaonyesha kuwa Shirki nidhambi kubwa, **alisema Mwenyezi Mungu mtukufu :{ Hakika Shirki nidhulma kubwa }** (Luqmaan 13).

Na alisema Mwenyezi Mungu mtukufu: **{ Na anaye mshirikisha Mwenyezi Mungu basi hakika amezua dhambi kubwa }** (An Nisaai 48).

{ Na anaye mshirikisha Mwenyezi  
Mungu basi huyo amepotea upotovu  
wa mbali }(An Nisaa 116)

Yote haya yanaonyesha kuwa  
ushirikina nidhambi kubwa, na itakapo  
kuwa ushirikina nidhambi kubwa  
kwahakika niwajibu kwa wana  
wachuoni na waliosoma kukataza  
nakutahadharisha watu wasiingie  
katika dhambi kubwa, na  
wasinyamanze, na niwajibu kuwapiga  
vita washirikina kama kuna uwezo  
wakufanya hivyo,kama alivyo wapiga  
vita Mtume (**S.a.w**).

Alisema Mwenyezi Mungu mtukufu:  
{ basi wauweni washirikina popote  
muwakutapo, na washikeni na

wazungukeni, na wavizieni katika kila njia. Lakini wakitubu, wakashika Sala, na wakatoa Zaka, basi waachilieni. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe **Mwenye kurehemu}** Al Tawbah-5 niwajibu kutahadharisha watu kutokana na ushirikina nakuwabainishia watu mpaka watakapo jiepusha na ushirikina, haya ndio yanayo paswa.

Ama kunyamanzia ushirikina na kuwaacha watu wana tanga tanga na kuingia katika ibada ya asie kuwa Mwenyezi Mungu, ilihali wanajidai kuwa niwaislam, na hakuna anae kataza wala hakuna anae hadharisha, basi hilo nijambo la khatari sana, kuna watu wanaelekea kwenye kukataza watu

wasile Riba, na zinaa, na kuharibika tabia, mambo haya yote niharamu na ndani yake kuna uovu, lakini Ushirikina ni zaidi, kwanini hawatilii umuhimu kuwakataza watu na shirki, na kubainisha yale yanayo tokea kwa watu wengi kutokana na kuingia katika shirki kubwa haliyakuwa wanajidai kuwa niwaislam.

Kwanini kuna kupuuzia katika jambo hili la ushirikina na kujighaflisha nakuwaacha watu wakiangukia katika shirki, ilihali kuna wanachuoni bali wanaishi pamoja nahao walio angukia katika shirki, na wana nyamanza?

Jambo la wajibu nikuelekea mmoja kwenda kukataza, hatari hii kubwa ambayo imeteketeza ummah vibaya,

Hakika kila dhambi isio kuwa shirki ninyepesi, lamsingi ni kuanza na jambo lenye umuhimu zaidi, kisha la chini yake.nk

### Maana ya Shirki.

Nikumuomba asie kuwa Mwenyezi Mungu pamoja na Mwenyezi Mungu Maana ya maneno hayo: Nikukipeleka kitu chochote katika ibada kwa asie kuwa Mwenyezi Mungu, kama Malaika, au Nabii au mtu mwema, au majini, au vitu vingine katika viumbe, ye yote mwenye kupeleka ibada kwa asiye kua Mwenyezi Mungu basi hili

ndilo jambo kubwa alilo kataza  
Mwenyezi Mungu, na ndio ushirikina.

Basi tambueni tafsiri ya Tawhiid na  
Shirki, kwasababu kuna baadhi yawatu  
wanatafsiri tawhidi kwatafsiri  
isiyokuwa yake na kuna anae tafsiri  
Shirki kwamaana isiyokuwa yake.

Kuna baadhi ya watu wanasema:  
hakika shirki ni shirki katika  
kuhukumiana, na maana hii imedhihiri  
katika zama hizi,

Kuhukumu kwa sheria isiokua ya  
Mwenyezi Mungu ninamna mionganii  
mwa namna za shirki na inaitwa shirki  
ya kutii(**Twaa**), hakuna shaka kwamba  
kumtii kiujabe katika kuhalalisha yale  
aliyo haramisha Mwenyezi Mungu au

kuharamisha yale aliyo halalisha  
Mwenyezi Mungu hii niaina ya shirki  
lakini kuna shirki kubwa kuliko hii,  
nayo ni kukiabudu kisicho  
kua Mwenyezi Mungu kwa kuchinja  
nakutoa nadhiri na kutufu nakuomba  
nusra,jambo la wajibu  
nikujitahadharisha na shirki zote  
asichukue aina moja ya shirki  
akaikataza kisha akaacha iliyo  
kubwa na yenye khatari zaidi, na  
asitaffiri maana ya shirki kuwa  
nikwenda kuhukumiana kwa  
asiyekuwa Mwenyezi Mungu basi, au  
maana ya shirki ni shirki katika siasa.

Na wengine wanasema: shirki katika  
makaburi nishirki nyepesi,maneno  
hayo nikufanya ujeuri kwa Mwenyezi

Mungu mtukufu, kwakua shirki ndilo jambo kubwa alilo likataza Mwenyezi Mungu,nalo nikukiomba kisichokuwa Mwenyezi Mungu pamoja na Mwenyezi Mungu.hii ndio Shirki.

Na miongoni mwao kuna anae sema:Shirki nikuipenda dunia na kuchukia mali.

Mali aliifanya Mwenyezi Mungu niyenye kupendwa mapenzi ya kikawaida na kitabia, anasema Mwenyezi Mungu mtukufu {Na mnapenda mali pendo la kupita kiasi} al fajri 20.

{Naye hakika bila ya shaka ana nguvu za kupenda mali! }**(Al Adiyat8)**

**Na amesema Mwenyezi Mungu**

{ Sema: Ikiwa baba zenu, na wanenu, na ndugu zenu, na wake zenu, na jamaa zenu, na mali mliyo yachuma na biashara mnazo ogopa kuharibika, na majumba mnayo yapenda, ni vipenzi zaidi kwenu kuliko Mwenyezi Mungu na Mtume wake na Jihadi katika Njia yake, basi ngojeni mpaka Mwenyezi Mungu alete amri yake. Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu wapotovu }  
**(Attawba 24).**

Alisema: kile mnacho kipenda zaidi, hakuwakataza waskipende,lakini alichو wakataza nikutanguliza mapenzi ya kitu hicho juu ya mapenzi ya kumpenda Mwenyezi Mungu, kupenda mali sio ushirikina, kwasababu hayo

nimapenzi ya kimaumbile, watu wanahitaji mali na wanapenda mali basi mtu kupenda mali sio ushirikina, kwasababu nikatika kupenda manufaa ambayo wanajinufaisha watu, lakini hao ambao wanao sema maneno hayo ima ni kwasababu hawajui hawakujifunza tauhiid na hawaijui shirki, au niwapingaji wanataka wawapeleke watu katika upotovu wakuto itambuwa Tawhiid na wafate matamanio ya nafsi zao, na Mwenyezi Mungu ndiye mjuzizaidi ya wanavyo kusudia.

Jambo lamsingi nikwamba hiyo sio shirki,kwasababu ushirikina nikumuomba asie kuwa Mwenyezi Mungu pamoja na Mwenyezi Mungu,

au kukipeleka kitu katika ibada kwa asie kua Mwenyezi Mungu, kama kuchinja na kutoa nadhri na kuomba dua nakuomba nusra na kuomba msaada nakukikimbilia kitu na kuogopa na kutarajia namengine mengi,

Kufanya hivyo ndio kuingia katika shirki ambayo ndiyo dhambi kubwa kwa Mwenyezi Mungu,kumuomba asie kuwa Mwenyezi Mungu kwasababu dua ndio aina kubwa ya ibada.

Anasema Mwenyezi Mungu mtukufu:  
**{Wa kuombwa kweli ni Yeye tu. Na hao wanao waomba badala yake hawawajibu chochote}.**(Araad)

na Anasema Mwenyezi Mungu  
mtukufu: {Basi mwombeni Mwenyezi  
Mungu mkimsafia Dini Yeye tu, na  
wangachukia makafiri} Ghaafir14.

Basi kukiomba kisicho kua Mwenyezi  
Mungu ni shirki ambayo  
ameiharamisha Mwenyezi Mungu na  
Mtume wake (s.a.w) ama haya baadhi  
ya vifungu wanavyo viweka baadhi ya  
watukatika kuelezea maana ya tawhid  
hivyo sio Shirki.

Tunaweza kusema kuwa hakika baadhi  
ya hivyo vifungu nisehemu katika  
shirki na katika hivyo kunavingine  
nihatari zaidi ya shirki, kwasababu  
shirki inatofautiana, baadhi yake ni  
mbaya zaidi kuliko nyingine,

tunaomba hifadhi kwa Mwenyezi  
Mungu.

**Dalili inayo onyesha kuwa Tawhiidi  
ni jambo kubwa alilo amrisha  
Mwenyezi Mungu.**

Amesema Mwenyezi  
Mungumtukufu: {Muabuduni  
Mwenyezi Mungu wala  
msimshirikishe na chochote } (An Nisaa  
36).

Aya hii ni dalili kubwa inayoonyesha  
kuwa jambo kubwa ambalo Mwenyezi  
Munguamewaamrisha waja wake ni  
Tawhid kisha ndio mambo mengine  
kama alivyo eleza katika Ayahii,  
Mwenyezi Mungu ameanza katika Aya  
hii kwa kuamrisha waja wake Tawhid

na akawakataza ushirikina, hii nidalili yakwamba Tawhid nijambo kubwa alilo amrisha Mwenyezi Mungu na ushirikina nijambo kubwa alilo likataza Mwenyezi Mungu.

Na Mwenyezi Mungu haanzi kuamrisha jambo ila linakuwa nikubwa na hakatazi jambo ila linakuwa nibaya, Mwenyezi Mungu huanza lamuhimu zaidi kisha linalo fuatia katika umuhimu.

**Ujumbe wa Nne Misingi mitatu ambayo ni lazima kuifahamu.**

Msingi wa kwanza: Kumtambua  
Mwenyezimungu Mtukufu:

Pindi pakisemwa kwako, **ipi misingi mitatu ambayo ni lazima kuitambua?**

**Basi sema:** Mja kumtambua Mola wake na dini yake na Mtume wake Muhammad (s.a.w).

Misingi: Mkusanyiko (**wingi**) wa msingi, na msingi ambao wenyewe kujengewa juu yake kitu kingine na tawi ambalo lenye kujengewa juu yake kitu kingine, basi kwa hivyo imeitwa misingi kwani inajengewa juu yake jambo la dini,. Na dini yote inazunguka juu ya misingi hii mitatu.

**Kwanini ameihuisha misingi hii mitatu?.**

Kwanini kwamba ndio misingi katika dini ya ki-islamu, na ni kwamba ni

maswali ambayo anaulizwa kwake mja pindi anapowekwa ndani ya kaburi lake, kwani hakika ya mja pindi anapowekwa ndani ya kaburi lake na pakasawazishwa juu yake udongo, na watu wakaondoka kutoka kaburini, hali wakirejea kwa jamaa zao, wanamjilia Malaika wawili ndani ya kaburi, basi kisha inarejeshwa roho yake katika kiwiliwili chake na anakua hai uhai wa maisha ya kaburini, sio kama maisha mfano wa maisha ya duniani, maisha ya Mwenyezi Mungu yeye mjuzi zaidi, **basi wanamuweka kitako** ndani ya kaburi lake na **kisha wanasema kumwambia yeye:** Nani Mola wako, na dini yako, **na Mtume wako?** **basi Muumini anasema:** Mwenyezi Mungu Mola wangu, na dini

yangu uislamu, na Muhammad  
(s.a.w)Mtume wangu, basi panasemwa  
kwake yeye: Vipi umefahamu?

Anasema: Nimesoma kitabu cha  
Mwenyezi Mungu nikatambua na  
kufahamu, basi anaita muitaji kwamba  
amesadikisha (amesema kweli) mja  
wangu basi mtandikieni katika pepo na  
mfungulieni yeye mlango katika pepo,  
na hutanuliwa kwake yeye kaburi lake  
urefu wa upeo wa jicho, na huletewa  
yeye harufu ya pepo na roho yake, basi  
anaangalia makazi yake katika pepo,  
**kisha anasema:** Ee Mola wangu  
simamisha kiama mpaka nirejee kwa  
watu wangu na mali zangu.

Na ama mwenye shaka ambae ameishi  
juu ya shaka na wasi wasi na kukosa

uyakinifu, na japokua anadai kua  
muislamu, pindi ikiwa kwake yeye  
kuna wasiwasi na Shaka katika dini ya  
mMwenyezi Mungu kama mnafiki,basi  
kwamba yeye anagagasia maneno,  
**(kujitafuna)** pindi pakisemwa kwake  
yeye: Nani Mola wako? Anasema  
sitambui, **na pindi pakisemwa:** Ipi dini  
yako?Anasema:sitambui,**na pindi**  
**pakisemwa:**Nani Nabii wako:  
Anasema sitambui haah haah hapana  
sitambui nimesikia watu wanasema  
kitu basi na mimi nikasema.

Yani katika dunia anasema yale  
yanayosemwa na watu pasi na imani  
ya kuamini tunamuomba Mwenyezi  
Mungu atulinde na hayo,huyu ni  
mnafiki ambae amedhihirisha uislamu

na hali yakua wala haitakidi  
**(kufungamanisha)** katika moyo wake,  
isipokua amedhihirisha kwake kwa  
ajili ya maslahi yake ya kidunia,**basi**  
**anasema:** katika dunia: Mola ni  
Mwenyezi Mungu, nae si mwenye  
kuamini hayo,**moyo wake unapinga**  
**tunamuomba Mwenyezi Mungu**  
atulinde na hayo!!**Anasema:** Dini yangu  
uislamu hali yakua haamini, **moyo**  
**wake unapinga!! Anasema:** Mtume  
wangu Muhammad (s.a.w) nae si  
mwenye kuamini ujumbe wa  
Muhammad katika moyo wake!!  
Hakika kwamba anasema katika  
kinywa chake tu**(ulimi)**, huyu ni  
mnafiki, **basi panasemwa kwake:**  
usingelijua,na ukasoma, basi anapigwa  
nyundo itokanayo na chuma, anapiga

kelele kutokana na maumivu laiti  
wangemsikia yeye vizito viwii(majini  
na wanadamu)wangezimia,  
wanamsikia kila kitu isipokua  
mwanadamu lau angelisikia  
angelizimia,kwamba:angekufa  
kutokana na uzito wake,na hubanwa  
ndani ya kaburi lake mpaka  
zinatofautina mbavu zake,na  
unafunguliwa kwake mlango wa  
motoni basi kisha inamjilia sumu yake  
na joto lake basi kisha anasema: Ee  
Mola wangu usisimamishe kiama,  
haya ni maisha yake na hali yake  
katika kaburi, tunamuomba Mwenyezi  
Mungu atulinde na haya, kwani  
hakujibu majibu yaliyo sahihi.

Pindi pakisemwa kwako: Nani Mola wako? basi sema: Mola wangu ni Mwenyezi Mungu ambaye alienilea na akalea walimwengu wote (**viumbe**) kwa neema zake.

Na kwa hivyo anaita muitaji kua kwamba umekanusha mja wangu basi mtandikie katika moto, na fungua kwake mlango katika moto, tunamuomba Mwenyezi Mungu atulinde, basi pindi ikiwa haya maswali kwa umuhimu huu inawajibika juu yetu tuwe ni wenye kujifundisha na kuitakidi nayo (**kua na imani nayo ndani ya moyo**) na wala haitoshi kujifunza pekee, bali kujifunza na kuitakidi na kuamini na kuyafanyia kazi, pale ambapo

tunadumu juu ya mfumo wa maisha,  
huenda Mwenyezi Mungu akawa  
mwenye kututhibitisha wakati wa  
maswali ndani ya kaburi.

Anasema Mwenyezi Mungu mtukufu:

(Mwenyezi Mungu huwathibitisha  
walioamini kwa kauli iliyo thabiti  
katika maisha ya dunia na katika  
akhera. Na Mwenyezi Mungu  
huwaacha kupotea hao wenye  
kudhulumu. Na Mwenyezi Mungu  
hufanya apendavyo)Ibrahim:27.

Basi hii misingi mitatu ina umuhimu  
mkubwa na kwa hivyo ni lazima  
kujengwa

Itikadi juu ya dalili za kitabu (Qur-ani) na Sunnah (Hadithi)na juu ya kuangalia katika Aya za Mwenyezi Mungu za kuumba,kwa ajili ya kua mwenye kusafisha akili na kuthibitisha katika moyo na kuondosha wasiwasi (shaka)Na ama itikadi zenyе kujengwa juu ya mifanano na na juu ya shaka na juu ya maneno ya watu, na ufuataji wa upofu,basi kwamba hakika ni itikadi zenyе kuondoka hazithibiti,nazo zinaelekewa na hatari ya kuvunjwa na kuelekewa na hatari ya kubatilishwa,

Basi hapathibiti itikadi na wala hukumu za kisheria zilizosalia isipokua kwa dalili Qur-ani na Sunnah na kwa dalili za akili zilizosalimika.

Pindi pakisemwa kwako kwamba:  
Umeulizwa nani Mola wako?na hili  
swali limepokewa utaulizwa kwake  
katika maisha ya dunia na akhera, basi  
lazima uwe unafahamu Mola wako  
mwenye ushindi na utukufu, na uwe  
mwenye kujibu kwa majibu yaliyo  
sahihi yenye kujengewa na uyakinifu  
na hoja,**basi sema:** Mola wangu ni  
Mwenyezi Mungu,hili ndilo jibu,  
ambae amenilea mimi na akalea wote  
walimwengu kwa neema yake hii dalili  
ya kiakili.

Basi Mola alietakasika na utukufu  
wake yeye ndiye ambae analea viumbe  
vyake wote kwa neema zake,

Katika matumbo ya mama zao umbile baada umbile katika viza(giza) vitatu,na kuwapatia kwao riziki mpaka katika matumbo ya mama zao,na kwa hivyo kinakua kiwiliwili cha mimba katika tumbo la mama yake na kua mkubwa,kwani inapata kwake yeye riziki kutoka kwa Mwenyezi Mungu alietakasika na utukufu wake, na inamfikia kwake yeye chakula.

Kisha panapulizwa ndani yake roho basi kisha anacheza na kua hai kwa idhini ya Mwenyezi Mungu haya ni malezi katika tumbo, kisha pindi akitoka basi hakika ya Mwenyezi Mungu subhaanah anamlea kwa uzima na afya na kumtambulisha juu yake maziwa ya mama yake,basi

anakunywa mpaka pale atakapokua  
mwenye kula chakula na akawa  
mwenye kutosheka na maziwa,kisha  
anakua kidogo kidogo mpaka anakua  
baleghe, kisha anakua na anakua  
mpaka anakua mtu mzima kisha  
anafikisha miaka arobaini,anakua  
mpaka mwisho wa kukua.

Basi ni nani ambae anamlisha toka  
siku ambayo amemuumba katika  
tumbo la mama yake mpaka kufikia  
kufa? nani ambae anamlisha kisha nani  
ambae anateremsha hiki chakula na  
hiki kinywaji katika kiwiliwili basi  
kisha kinafika katika kila viungo na  
kwenda katika kila sehemu katika  
kiwili wili,nani ambae anamtamanisha  
kwake ye ye chakula na kinywaji, nani

ambae humgeuza na kumtoa kwake madhara kwake, nani ambae anafanya haya na kumlea huyu mwanadamu, hivi haikuwa Mwenyezi Mungu alietakasika na utukufu wake? Huyu yeye Mwenyezi Mungu alietakasika na utukufu wake ambae anamlea, yeye ambae amenilea mimi na akalea walimwengu wote kwa neema zake.

Na yeye ni mwenye kumuabudu mimi hapana kwangu mimi mwenye kumuabudu isiokua yeye.

Kila ambae yupo juu ya sura ya ardhi katika ulimwengu wa wanaadamu na wanyama, na ulimwengu wa nchi kavu na baharini, kutoka viumbe wakubwa mpaka kufikia viumbe wadogo, katika

nchi kavu na baharini wote wanakula  
kwa neema zake na riziki  
yake,**amesema Mwenyezi Mungu**  
**Mtukufu:** (Au ni nani huyo ambaye  
atakupeni riziki kama Yeye akizuia  
riziki yake?)**Almulk:** 2. **Na akasema:**  
(Na hakuna mnyama ye yote katika  
ardhi ila riziki yake iko kwa Mwenyezi  
Mungu.Naye anajua makao yake na  
mapito yake) **Hud:6.**

**Na akasema:** (Na wanyama wangapi  
hawawezi kujimiliki riziki zao!  
Mwenyezi Mungu anawaruzuku hao  
na nyinyi pia. Na yeye ndiye Mwenye  
kusikia Mwenye kujua) **Huyu, yeye**  
**Mwenyezi Mungu alitakasika:**(Huyo  
ndiye Mwenyezi Mungu,Mola wenu  
Basi muabuduni yeye) **Yunus:3.**

Ama asiekua Mwenyezi Mungu mwenye ushindi alietakasika akawa juu basi hamiliki kwake chochote si masanamu na wala kinginecho hapana mmoja yejote anamiliki katika riziki kitu isipokua yeye anaruzukiwa, kiumbe mfano wako.

Na yeye Mwenye kuabudiwa: Mola ambae hili jambo lake yeye ambaeanastahiki ibada kwangu mimi na mwengineo haitoshi kukubali tu kua yeye kwa Uungu (**kwamba Muumbaji**)haitoshi kua mwenye kusema Mola wangu ni Mwenyezi Mungu ambae alienilea kwa neema zake.

Hii haitoshi hapana budi kua mwenye  
kukubali kwake yeye kwa uabuduji, na  
kutakasa kwake kwa ibada, nahii ndio  
tofauti kati ya mpwekeshaji na  
mshirikina, mpwekeshaji anakiri kwa  
Ungu wake Mwenyezi Mungu  
mwenye ushindi na utukufu na  
uabudiwaji wake pekee usio kua na  
ushirikina kwake, Na mshirikina  
anakiri kwa Uungu wa Mwenyezi  
Mungu, lakini yeye mshirikina katika  
ibada zake Mola, anashirikisha pamoja  
nae mwengine katika ibada zake,  
anashirikisha pamoja nae  
ambaeasieumba wala kuruzuku na  
wala hamiliki chochote, hii ndio tofauti  
kati ya amabae ni mpwekeshaji na  
mshirikina, **Mpwekeshaji anasema:**  
Mola wangu ni Mwenyezi Mungu,

nae namuabudu, na hapana kwangu  
mimi kinyume chake, **ama mshirikina**  
**basi anasema:** Mola ni Mwenyezi  
Mungu, lakini ibada kwake yeye si  
maalumu kwa Mwenyezi Mungu,  
basi anaabudu pamoja na Mwenyezi  
Mungu miti na mawe na mawalii na  
wema na makaburi, basi kwa hivyo  
anakua mwenye kushirikisha na wala  
haimnufaishi kwake yeye kukubali  
kwake na kukiri kwa Mwenyezi  
Mungu na wala hajaingia katika  
uislamu.

Nae Mwenye kuabudiwa, kwamba  
Mwenyezi Mungu ambae namuabudu.

Hapana kwangu muabudiwaji isipokua  
yeye: si katika Malaika na wala katika

Mitume na wala katika wema (**waja**) na wala katika miti na wala katika mawe na wala katika kitu chochote, hapana muabudiwa kwangu kinyume chake alietakasika na utukufu wake, hii ni kukubali tawhidi kwa dalili, na hii dalili ya akili, kisha kataja dalili ya kisomi kutoka ndani ya Qur-ani, **na dalili tamko lake Mtukufu:** (**Kila sifa njema anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe wote**) Alfaatiha:2.

Hii aya ambayo ipo mwanzo wa Qur-ani katika msahafu, hapana kabla yake isipokua kwa jina la Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema mwenye kurehemu, nalo tamko la mwisho la watu wa peponi, **amesema:**

(Na mwisho wa wito wao ni:  
Alhamdu lillah Rabbil alamiin  
“Kuhimidiwa kote ni kwa Mwenyezi  
Mungu, Mola wa walimwengu  
wote”)na Mwenyezi Mungu mtukufu  
ameanza kwake(**kueleza**)uumbaji,  
**amesema mtukufu:**(Sifa njema zote ni  
za Mwenyezi Mungu alie umba  
mbingu na ardhi, na akafanya giza na  
mwangaza) **An-aam:1,**

Na kisha akamalizia kwake (**maelezo**)  
kwa kuumba **amesema Mtukufu**  
**Mwenyezi Mungu:** (Na patahukumiwa  
kati yao kwa haki na patasemwa:**Sifa**  
zote njema anastahiki Mwenyezi  
**Mungu, Mola wa viumbe vyote)**  
**Azzumar:75.**

Basi alianza kwake kwa kuumba na kumalizia kwake kwa kuumba basi hilo tamko kubwa.

Na mpaka mja(**kiumbé**)akikutimizia (**akikutekelezea**) kitu kwako katika ihsani basi kwamba hayo yanatokana kwa Mwenyezi Mungu,yeye ndiye ambae amedhalilisha kwako huyu kiumbe,nae ambae aliemuwezesha kua mwenye kufanya uzuri kwako,basi shukrani zinarejea kwa Mwenyezi Mungu alietakasika na utukufu wake.

Na Mwenyezi Mungu: maana yake:ni mwenye Uungu na kuabudiwa juu viumbé vyake vyote, na hili jina halitamkwi isipokua kwake yeye tuu

subhaanah, hapana yeote mwenye  
kujiita Mwenyezi Mungu,**hata firauni  
hakupata kusema:** mimi Mungu,  
isipokua kasema mimi mola wenu,basi  
jina ni maalumu tu kwa Mwenyezi  
Mungu, hapana mmoja yeote  
mwenye kujiita kwake yeye na wala  
mmoja yeote mwenye ushupavu wa  
kusema mimi ni Mwenyezi Mungu.

Basi ni wazi kwamba shukrani zote na  
sifa zote ni kwa Mwenyezi Mungu  
Mola wa viumbe wote.

Na ulimwengu wa Malaika na  
ulimwengu wa vitu na vyote vikavu na  
ndege na ulimwengu wa wanyama  
wakali na ulimwengu wa wanyama  
wasio wakali na ulimwengu wa

wadudu na vidudu, ulimwengu katika nchi kavu na baharini hakuna ajuae isipokua Mwenyezi Mungu na hapana mdhibiti isipokua Mwenyezi Mungu vyote Mwenyezi Mungu ndiye bwana wao na Mola wao.

Mola wa walimwengu: na hili haliitwi isipokua juu ya Mwenyezi Mungu mwenye ushindi mtukufu,**haiwezekani kwa ye yote awe mwenye kujisema kwake yeye:** Mola wa walimwengu.

Pindi pakisemwa:**Mola:Basi hii** hapaitwi isipokua juu ya Mwenyezi Mungu,juu ya Mwenyezi Mungu mtukufu aliye juu,wala hapageukwi isipokua kuelekea kwake, ama viumbe panafungamanishwa, **basi kusemwa:**

mlezi wa nyumba,mlezi wa wanyama,  
**kwamba:**mfalme wao na rafiki yao.

Na yote hapana isipokua Mwenyezi  
Mungu katika ulimwengu, na mimi ni  
mmoja katika huo ulimwengu.

Na yote hapana isipokua Mwenyezi  
Mungu katika ulimwengu,na mimi ni  
mmoja katika huo ulimwengu, basi  
inakua Mwenyezi Mungu Mola  
wangu, kwani Mwenyezi Mungu ni  
Mola wa walimwengu,na mimi ni  
mmoja katika huo ulimwengu, **basi**  
**hapana yejote anaweza kua mwenye**  
**kusema:**Na mimi ni Mola asiyekua  
Mola wa walimwengu, si kwa kafiri  
wala muislamu, hili haliwezekani  
milele na wala hasemi mwenye akili,

hii ni dalili juu ya Uungu wake  
Mwenyezi Mungu mwenye ushindi  
mwenye kutukuka, na kwakua  
kwamba hakika yeye ni Mola wa  
walimwengu basi yeye anastahiki  
kuabudiwa, **na hii inabatilisha ibada**  
**isiokua yeye aliyetakasika na utukufu**  
**na kwahivyo kasema baada yake:**  
(Wewe peke yako ndiye tunaekuabudu  
na wewe peke yako ndiye  
tunaekuomba msaada) Alfaatiha:5

Na ibada haikubaliki isipokua pamoja  
na kukanusha na kuthibitisha, nayo ni  
maana ya Laa IlaaHa illa llah (**Hapana**  
**Mola ambae anaestahikiwa kuabudiwa**  
**kwa haki isipokua Mwenyezi Mungu**)  
ndani yake kuna kukanusha na  
kuthibitisha, kupinga Uungu usiokua

wa Mwenyezi Mungu, na kuthibitisha kwake kwa Mwenyezi Mungu mwenye ushindi na utukufu.

Pindi pakisemwa kwako: Kwa vipi unamtambua Mola wako? Basi sema:  
Kwa dalili zake na viumbe wake.

Wewe umesema: Mwenyezi Mungu  
Mola wangu au Mola wangu  
Mwenyezi Mungu ambae ni mlezi  
wangu kwa neema zake, **ni ipi dalili**  
**juu ya kwamba Mwenyezi Mungu ni**  
**Mola wako ambae amekulea kwa**  
**neema zake?** pindi pakisemwa kwako:  
kwa lipi unamtambua Mola  
wako?kwani kwamba mwenye kudai  
kitu basi hapana budi awe mwenye  
kusimamisha hoja juu ya madai yake.

Wadaiji pindi si wenyе kusimamisha  
\*\* juu yake hoja watu wake watamdai

Hapana budi kwa kila mdaiji awe  
mwenye kusimamisha dalili juu ya  
madai yake, kinyume chake itakua  
madai yake sio sahihi, **wewe umesema:**  
Mola wangu ni Mwenyezi Mungu  
ambae ni mlezi wangu na mlezi wa  
walimwengu wote kwa neema zake, **ipi  
dalili? basi sema:** Dalili ni Aya zake na  
viumbe wake.

Aya zake, **kwamba:** Alama zake na  
dalili zake zijulishazo juu yake  
subhaanah (**aliyetakasika na utukufu  
wake**) basi viumbe vyote ambavyo  
unavyoviona vyote vilikua havipo  
kisha Mwenyezi Mungu akavifanya

viwepo na akaviumba kwa uwezo  
wake aliyetakasika na utukufu.

Na kwake yeye ameumba vinapatikana  
mfano wa mimea na vizaliwavyo na  
vitu havikui vyenye kupatikana kisha  
vikapatikana na hali yakua mkawa  
mnaangalia hivyo kwake, nani ambae  
anaumba kwake? ni yeye Mwenyezi  
Mungu alietakasika na utukufu.jee  
vinajiumba vyenyewe,jee mmoja  
yeyote katika watu ameumba? hapana  
yeyote mwenye kudai haya, na wala  
hawezi kudai. **Amesema Mwenyezi**  
**Mungu Mtukufu :**(Au wao  
wameumbwa pasipo kutokana na kitu  
chochote,au ni wao ndio waumbaji? \*\*  
Au wao wameziumba mbingu na

ardhi? Bali hawana yakini) At-tuur 35-36

Hivi vitu si vyenye kujipatisha  
vyenyewe au amevipatisha  
mwenginewe katika viumbe kamwe,  
haikua na wala haiwi anaumba yejote  
mti au mbu au nzi: (Hakika wale mnao  
waomba kinyume na Mwenyezi  
Mungu,hawatouumba hata nzi japo kua  
watajumuika kwa hilo)Alhajj:73.

Basi huu uumbaji unajulisha juu ya  
Muumbaji Subhaanah mtukufu, na  
kwa hivyo pindi paliposemwa  
kuambiwa mwarabu mbedui juu ya  
mshangao: Vipi unamtambua Mola  
wako? Ngamia anajulisha juu ya  
ngamia, na athari inajulisha juu ya

mtembeaji, hivi haijulishi huu  
ulimwengu juu ya alie Mpole Mjuaji?.

Pindi ukiangalia alama za nyayo juu ya ardhi, hivi haikujulishi haya juu ya kwamba kuna mmoja ametembea juu ya hii ardhi? Na pindi ukiangalia kanyago za ngamia hivi haikujulishi?.

Na katika dalili zake usiku na mchana jua na mwezi, **na katika viumbe wake:** mbingu saba na ardhi saba na vilivyomo ndani yake na kati yake.

Hii hakika kwamba inajulisha ardhi ndani yake kuna ngamia au kapita juu yake ngamia, nakanyago inajulisha juu ngamia na alama inajulisha juu ya mtembeaji.

Na katika dalili zake usiku na mchana  
jua na mwezi:na Aya zimegawanyika  
sehem mbili: kigawanyo cha kwanza:  
Dalili za ulimwengu zinaonyesha,  
mfano wa mbingu na ardhi na nyota  
jua na mwezi na majabali miti na  
bahari, zimeitwa ni alama,kwani  
kwamba zinajulisha juu ya muumbaji  
alietakasika na utukufu wake,na kwa  
hivyo anasema Abuu l- **ataahy katika  
shairi zake:**

Basi hushangai vipi anaasiwa  
Mungu\*\*ama vipi anapinga mpingaji

Na katika kila kitu kwake ni dalili \*\*  
inajulisha kwamba ni mmoja

Na kwa Mungu kila kitu  
kitingishikacho \*\* na kituliacho katika  
nyuma angalia.

Vipi anapinga mmoja Mwenyezi  
Mungu alietakasika na utukufu  
anasema:Hakuna huko Mola kwa huu  
ulimwengu wote, na hivi viumbe  
vimepatakina pasi na muumbaji,**na**  
**vikipatikana na muumbaji basi nani**  
huyu muumbaji isiyokua Mwenyezi  
Mungu aliemtukufu nibainishie mimi?  
hautokuta muumbaji asiokua  
Mwenyezi Mungu alietakasika na  
utukufu wake: (Au wamemfanyia  
Mwenyezi Mungu washirikia  
waliouumba kama alivyoumba yeye, **na**  
**viumbe hivyo vikawadanganyikia?**  
Sema: Mwenyezi Mungu ndie

Muumba wa kila kituna yeye ni mmoja  
mwenye kushinda) Ar-raadi:16.

Kigawanyiko cha pili: Dalili za qur-ani  
ambazo zinasomwa kutoka katika  
wahyi wa mshushaji juu ya Mtume  
(s.a.w.)hizi zote dalili juu ya  
kupatikana Mwenyezi Mungu  
alitakasika na utukufu wake, na juu ya  
ukamilifu wake na sifa zake na majina  
yake na juu ya kwamba anastahiki kwa  
ibada pekee pasi na mshirika kwake,  
yote yanajulisha juu ya aya za  
ulimwengu na aya za qur-ani.

Na dalili za ulimwengu zilizopo  
zinajulisha juu yake kwamba yeye  
muumbaji na mpatishaji na  
mwendeshaji ulimwengu,na dalili za

qur-ani ndani yake kuna amri za kuabudu Mwenyezi Mungu, na ndani mna kukiri kupwekeka kwa umola wake, kila qur-ani inazunguka katika maana hii, na kuteremshwa katika hii maaana.

Na katika aya zake usiku na mchana jua na mwezi, hii ni katika dalili kubwa alietakasika na utukufu wake, usiku wa kiza ambao unafunika huu ulimwengu, na mchana wenye kung'ara ambao unang'arisha huu ulimwengu, **basi kisha watu wanashughulishwa amesema mtukufu:** (Sema: Mnaonaje, Mwenyezi Mungu ange ufanya usiku ubakie moja kwa moja mpaka siku ya Kiyama, mungu gani asiye kua Mwenyezi Mungu

atakye kuleteeni mwangaza?Basi je hamsikii? Sema:Mnaonaje, Mwenyezi Mungu ange ufanya mchana ubakie moja kwa moja mpaka siku mpaka siku ya Kiyama, mungu gani asiye kua Mwenyezi Mungu atakaye kuleteeni usiku mkapumzika humo? Basi je hamuoni? Na kutokana na rehema zake amekujaalieni usiku na mchana mpare kupumzika humo na mtafute fadhila zake, na ili mpare kushukuru)  
Alqaswas:71-73

Hii ni katika dalili kubwa za Mwenyezi Mungu huu mchana na usiku, na si mda wote usiku, na si mda wote mchana, kwani kwamba lau ingelikua hivyo hivyo tuu

yangeharibika maslahi ya waja na  
wangechoka.

Amefanya Mwenyezi Mungu kwao  
usiku na mchana vinafuatana, kisha  
usiku na mchana vimepangiliana  
haendi kinyume mmoja yejote na wala  
hapabadiliki, juu ya mpango mmoja  
katika unaojulisha juu ya hekima wa  
Muhukumu alietakasika na utukufu  
wake, vitendo vya waja havibadiliki na  
vitendo vyao vinaharibika na  
kutofautiana vyovyote iwayyo na  
kuharibika, ama viumbe wa Mwenyezi  
Mungu basi kwamba hapaharibiki  
isipokua kwa mda anaoruhusu  
Mweneyzi Mungu kwamba paharibike  
kwake.

Mchana na usiku vyenye kuendelea hapaharibiki kimoja wapo, ama pale katika utengezaji wa kiumbe panaharibika na kubomoka na kwisha ijapokua ngumu na kubwa.

Kama manvyoona katika magari yatemebeayo na ndege na meli pamoja kwamba vina nguvu na kutiliwa nguvu kwake lakini vianaharibika na kubomoka, jee umeharibika usiku au mchana? Hapana, **kwani kwamba mtengenezaji wake mwenye uwezo mwenye hekima alietakasika na utukufu wake:** (Huo ndio ufundi wa **Mwenyezi Mungu alietengeneza vilivyo kila kitu**) An-namli:88.

Na dalili juu Umola wake na Ungu wake (**wakuabudiwa**) alietakasika na utukufu wake

Na dalili tamko la Mtukufu: (Na katika aya zake ni usiku na mchana, na jua na mwezi, basi msilisujudie jua wala mwezi, bali msujudieni Mwenyezi Mungu alie viumba, ikiwa nyinyi mnamuabudu Yeye tu) Fuswilat:37.

Hii dalili juu Umola wake na Ungu wake wa kuabudiwa subhaanah wata-aalah: (Na katika aya zake ni usiku na mchana, na jua na mwezi).

Jua na mwezi: Jua ni sayari kubwa ambayo inaangaza ulimwengu na kupatisha joto kama alivyotamka Mwenyezi Mungu mtukufu: (Na

tukaifanya taa yenye mwanga na joto)  
Annabai:13.

Na mwezi ni nuru unaangaza usiku na  
unaangaza njia kwa watu,na katika  
maslahi yake viwili hivyo pia  
kutengeza ulimwengu kwa miti yake  
na matunda yake na bahari yake, basi  
lau Jua likajificha katika ulimwengu  
ungeharibika ulimwengu na  
pangeharibika mengi katiak maisha ya  
watu na maslahi yao, na ungelijificha  
mwezi hivyo hivyo, na mwezi pia  
ndani mna manufaa kwa matunda na  
miti, pamoja yale yaliopo ndani yake  
vile vile katika kutambua hesabu ya  
kalenda,**amesema mtukufu:** (Na mwezi  
ukawa na nuru,na akaupimia vituo ili

mjue idadi ya miaka na hesabu)  
Yunusu:5.

Na amesema: (wanakuuliza khabari ya mwezi(mwandamo).Sema hiyo ni vipimo vya nyakati kwa ajili ya watu na hija) Albaqara:189.

Basi katika mwezi kuna masilahi ya kutambua nyakati na muda,muda wa madeni, na muda wa hesabu za desturi za wanawake (**hedhi**) na nyakati za ibada na funga na hija, **vyote vinatambulika kwa hesabu inayojengewa juu ya hizi nuru mbili:** Juana mwezi,basi hesabu ya jua na hesabu ya mwezi basi ndani yake kuna maslahi ya viumbe wote.

Na katika viumbe wake mbingu saba amesema mtukufu: (Mwenyezi Mungu ni yule ambaye ameziumba mbingu saba, na ardhi kwa mfano wa hiso) Attalaaq 12.

(Alieumba mbingu saba kwa matabaka). Almulk: 3.

Baadhi yake juu baadhi ya nyengine, mbingu ya dunia kisha ambayo inayofuata mpaka kufikia ya sabana juu ya vyote kuna kiti chake cha enzi (arshi) Mwenyezi Mungu alietakasika na utuku wake.

Na ardhi saba kama alivyosema mtukufu : (Na ardhi kwa mfano wa hiso) Basi ni matabaka saba vilevile na kila tabaka katika matabaka ya mbingu

saba na ardhi saba ina wakazi na majengo, ila katika mbingu kuna nyota na sayari mwezi na jua, na ila katika ardhi kuna viumbe katika wanyama kwa kutofautiana namna zake na katika majabali na miti na mawe na madini na bahari hizi ni alama za Mwenyezi Mungu mtukufu alietakasika, dalili za kiulimwengu ambazo huonwa na kushuhudiliwa.

Amesema rehema za Mwenyezi Mungu zimwendee:na dalili kauli ya Mwenyezi Mungu mtukufu: (Na katika aya zake ni usiku na mchana, na jua na mwezi, basi msilisujudie jua wala mwezi, bali msujudieni Mwenyezi Mungu alie viumba, ikiwa nyinyi mnamuabudu Yeye tu) Fuswilat:37.

Katika aya zake usiku: yani katika alama zake zижلیحازو جوو یا Ungu wake na uwezo wake na kwamba anastahikiwa kwa ibada kinyume na mwengine usiku ambao unatia kiza na mchana ambao unaangaza ulimwengu mzima, hii ni katika maajabu ya alama za Mwenyezi Mungu alietakasika na utukufu wake.

Basi ni nani ambaye anafanya ulimwengu wote kiza katika mda mmoja? kisha anafanya ulimwengu mwangaza katika wakati mmoja?ni Mwenyezi Mungu alietakasika na utukufu wake.lau pangelikusanyika viumbe juu ya kwamba waangaze nuru sehemu katika ardhi wasingeliweza kua wenye kuangaza nuru isispokua ni

sehemu zenyе mipaka maalumu,lau wangelikuja na umeme ambao upo katika dunia yote hauangazi isipokua sehemu maalum katika ardhi.

Ama jua na mwezi viwili hivi vinaangaza ardhi yote, usiku na mchana unafuatana na jua na mwezi vile vile.

Amesema mwenyezi Mungu:  
**(Msilisujudie jua wala mwezi, bali msujudieni Mwenyezi Mungu alie viumba,ikiwa nyinyi mnamuabudu Yeye tu) Fuswilat:37.**

Hii ni ubatilifu kwa washirikina,msisujudie kwa viumbе,kwani katika ukubwa wa viumbе jua na mwezi, na kwamba

washirikina ilikua wanaabudu jua na kusujudia, na mionganini mwao wapo wanaabudu makaburi na nyota mfano watu wa Ibrahim (Nabii) wanajenga kwake hekalu juu ya sura nyota na kuabudia kwake, **basi tamko lake mtukufu: (Msilisujudie jua)** sijida maana yake kuweka bapa ra uso juu ya ardhi kwa unyenyekevu, nalo kubwa katika namna za ibada, anasema Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w): ((Ukaribifu zaidi unakua kati ya mja na Mola wake nae katika hali ya sijida)).

Basi ukubwa wa namna za ibada kusujudu juu ya ardhi, kwani uso wako ambao ni kitu kitukufu kwako umeweka kwa Mwenyezi Mungu hali ukiabudu na kunyenyekea kati ya

mbele ya Mwenyezi Mungu  
alietakasika na utukufu,huku ndio  
kusujudu kwa hakika,na haifai  
isipokua kuabudu kwake yeye  
Mwenyezi Mungu pekee.

Ama kusujudia jua na mwezi basi  
kusujudu kwa viumbe haistahiki kua ni  
vyenye kusujudiwa kwake,basi haifai  
kusujudia viumbe,isipokua kwamba  
kusujudu kwa muumbaji viumbe,ama  
viumbe basi mfano wako viumbe  
vinaendeshwa na kuamrishwa,jee  
unasujudia kiumbe kinachoshindwa  
mfano wako? hii haifai, wapi akili  
zako zimeenda?!!.

Na tamko lake Mwenyezi Mungu:  
**(Hakika Mola wenu ni Mwenyezi**

Mungu aliye ziumba mbingu na ardhi  
katika siku sita,kisha akatawala juu ya  
kiti Cha enzi, huufunika usiku mchana,  
ufuatao upesi upesi, na jua na  
mwezi,na nyota zinazo tumika kwa  
amri yake, fahamuni kuumba na amri  
ni yake,ametukuka kabisa Mwenyezi  
**Mungu, Mola wa viumbe vyote)**  
Aaraaf:54.

Kusujudu ni kwamba kunastahiki kwa  
muumba alietakasika na utukufu wake  
ambaye hashindwi na chochote,basi  
kusujudu ni haki kwa Mwenyezi  
**Mungu alietakasika na utukufu wake**  
na hapana haki kwa viumbe vyovyote  
imekua huyu kiumbe ana ukubwa na  
utukufu basi kwamba kiumbe ni dhaifu  
mwenye kuendeshwa na mwenye

kuamuliwa kwake (Basi msilisujudie  
jua wala mwezi bali msujudieni  
Mwenyezi Mungu aliye viumba ikiwa  
nyinyi mnaabudu yeye tu) fuswilat:37.

Basi lililo wajibu kwamba tusiwe  
wenye kuabudu isipokua Mwenyezi  
Mungu,pindi mkisujudu kwake na  
mkasujudu kwa mwenginewe basi  
inakua nyinyi mnaabdu kwa Mwenyezi  
Mungu ibada iliyo sahihi,bali  
mnaabudu pamoja na kufanya  
ushirika,na ushirika(shirki)unaharibu  
ibada.

Hakia ya Mola wenu, **kwamba:** yule  
aliekuumbeni na akakutunzeni kwa  
neema zake, hapana Mungu apasae

kuabudiwa kwa haki ila yeye  
alietakasika na utukufu wake.

Kisha akataja dalili juu ya hayo basi  
akasema: (**Ambae ameumba mbingu  
na ardhi**) Aaraaf:54.

Hii ni hoja juu UNGU wa Mwenyezi  
Mungu mwenye ushindi  
alietu kuka, kwamba ameumba mbingu  
na ardhi, na hapana ye yote ameumba  
kitu katika viwili hivyo, na wala  
mmoja ye yote amemsaidia  
alietakasika na utukufu wake juu ya  
hilo, bali ye yeye amepwe keka kwa  
vi umbe wake (**Ameumba mbingu na  
radhi**) jee kuna mmoja katika  
washirikina au wapingaji  
(**wakengeukaji**) anap pinga hili na

kusema:Hajaumba Mwenyezi Mungu  
mbingu wala ardhi,ambae alieumba  
viwili hivi Fulani, au mimi ndie  
nilieumba,au ameumba sanamu fulani?  
jee amesema haya mmoja katika  
ulimwengu wa mwanzo na wa  
mwisho, pamoja kwamba hii aya  
inasomwa usiku na mchana? wala  
hakuna mmoja yejote anapinga na  
hawezi kupinga milele.

Katika siku sita:Hivi viumbe vikubwa  
ameviumba Mwenyezi Mungu katika  
siku sita,nae ni muweza juu ya kuumba  
katika mda mmoja tu,lakini ameumba  
katika siku sita kwa hekima anajua  
yeye alietakasika na utukufu, na  
masiku sita mwanzo wake siku ya  
jumapili na mwisho wake siku ya

ijumaa,katika siku ya ijumaa  
pamekamilika uumbaji, na kwa hivyo  
imekua hii siku kubwa katika masiku  
ya wiki, nayo ni bwana wa masiku na  
idi ya wiki siku hii,nayo ni siku bora.

Amesema Mjumbe wa Mwenyezi  
Mungu (s.a.w): ((Bora ya siku  
iliyochomoza kwake jua siku ya  
ijumaa)) kwani kwamba  
pamekamilika kwake kuumba  
viumbi,na kuumbwa kwake Adamu na  
kuingizwa peponi na kutolewa  
(kuteremshwa) kwake,na siku ambayo  
kwake itatokea kiyama,yote hayo siku  
ya ijumaa, basi siku ilo bora kwa  
masiku,nayo siku ya mwisho  
kuumbwa kaumba mbingu na ardhi na  
vilivyomo ndani yake.

(Hakika Mwenyezi Mungu ndiye  
anaye zuilia mbingu na radhi  
zisianguke.Na zikidondoka hapana  
yeyote wa kuzuzuia isipo kua Yeye.))  
Faatir:41.

Basi kitiki cha enzi ni muhitaji kwa  
Mwenyezi Mungu mwenye ushindi  
alietukuka kwani kwamba yeye  
muumbwa (**arshi**),na Mwenyezi  
Mungu ni mkwasi (**tajiri**) kutokana na  
arshi(**kitiki cha enzi**)na  
venginevyo,lakini yeye Mwenyezi  
Mungu ametengemaa juu yake kwa  
hekima anajua yeye alietakasika na  
utukufu,na kutengemaa ni namna  
katika ujuu (**kutukuka**) lakini kua juu  
sifa ya nafsi (**pekee**), ama kutengemaa  
basi sifa amefanya na anafanya

anapotaka alietakasika na utukufu  
wake.

(Unaufunika usiku mchana) kwamba  
unaufunika usiku mchana,na  
unaufunika mchana usiku basi pale  
ambapo unaona ulimwengu unaangaza  
mwanga basi pindi tu  
usiku unaufunika na unakua giza.

Na usiku unaufunika mchana unakua  
unaangaza (**uanutafuta haraka**) inakuja  
hii baada hii papo kwa papo pasi na  
kuchelewa,basi pindi ukigeuka usiku  
umekuja mchana,na pindi ukigeuka  
mchana umekuja usiku papo kwa papo,  
hapachelewi huu kwa huu,na hii ni  
katika ukamilifu wa alietakasika na  
utukufu wake,haidhoofishi hii

kutokana na hii,na jua ni sayari kubwa  
iliyo maarufu na mwezi vile vile sayar  
katika sayari saba zitembeazo na kila  
katika viwili hivyo vinatembea na  
kuzunguka juu ya ardhi.

Na nyota:nayo ni sayari,yenye  
kudhalilishwa kwa amri  
yake,kudhalilishwa katika kutembea na  
kuzunguka daima na wala  
hazichelewi,na hii marejesho ya  
majibu juu ya wale ambao wanaabudu  
jua na mwezi na nyota kwamba  
vimedhalilishwa kwa amri ya  
Mwenyezi Mungu  
vimeamrishwa,Mwenyezi Mungu  
ambaye anavipitisha,na Mwenyezi  
Mungu ambaye anavisimamisha pindi  
akitaka alietakasika na utukufu wake,

basi yeye mdhoofishaji muendeshaji  
hapana kwake yeye katika kitu amri  
yoyote.

Kuumba:Nako ni kupatisha basi yeye  
Muweza juu ya viumbe pindi akitaka  
alietasika na utukufu wake anaumba  
kile atakacho.

Na amri: Ameamrisha alietakasika na  
utukufu wake,

Ameamrisha ulimwengu: Ambaye  
anaamrisha kwake yeye viumbe basi  
vinatii na kuitikia kwake mfano wa  
tamko lake: (**Akaziambia** hizo na  
**ardhi: Njooni** kwa khiyari au kwa  
**nguvu**) Fusilat:11. ameamrisha hizo  
alietasika na utukufu, na hii amri ya  
ulimwengu ameamrisha kwake mbingu

na ardhi basi zikatengenezeka, (Hakika  
amri yake anapotaka kitu kitu ni  
kukiambia tu,Kuwa! Na kikawa)  
Yasini:82, hii amri ya kiulimwengu.

Ama amri ya kisheria:Basi nayo ni  
ufunuo (**wahyi**) unaoshushwa ambae  
anaamrisha kwake waja wake,  
anawaamrisha kwa kumuabudu  
kwake,anawaamrisha kwa swala,  
anawaamrisha kwa zaka,anawaamrisha  
kwao kuwafanyia wema wazazi  
wawili,hii amri ya kisheria,panaingia  
ndani yake amri nyingi na makatazo  
mengi ambayo katika qur-ani na  
hadithi za Mtume (**s.a.w**) zilizo  
sahihi,hii katika amri ya Mwenyezi  
Mungu alietakasika na utukufu wake.

Ikiwa kwake kuna uumbaji na amri  
basi kitu gani kimesalia kinginecho  
isiyokua alietakasika na utukufu wake?  
na kwa hivyo anasema Ibnu Omari  
pale aliposoma hii  
aya,**kasema:** Mwenye kitu basi  
aamrishe.

Na Mola ni mwenye kuabudiwa,**na**  
**dalili tamko lake mtukufu:** (Enyi  
watu! Muabuduni Mola wenu ambaye  
amewaumbeni ninyi na wale  
waliyokuwa kabla yenu; ili  
kuokoka. Mwenyezi Mungu ambaye  
aliyewafanyia ardhi hii kama  
tandiko, na mbingu kama paa na  
akateremsha maji kutoka  
mawinguni, na kwa hayo akatoa  
matunda yawe riziki kwenu, Basi

msimfanyie Mwenyezi Mungu  
washirika,ili hali mnaelewa.)  
Albaqarah:22.

Mola wa walimwengu: Mfano wa  
yaliyotangulia basi katika hii aya ni  
kukiri upwekesho,upwekesho wa  
uumba na upwekesho wa Ungu kama  
namna ilivyotangulia,

Na Mola mwenye kuabudiwa,kwamba  
ye ye ambaye anastahiki ibada,ama  
mwengineyo hastahiki ibada,kwani  
kwamba si Mola,kisha vile vile  
haitoshi kwamba mwanadamu anakiri  
kwa Uumba wake Mwenyezi Mungu  
bali lazima awe anakubali kuabudu  
kwa Mwenyezi Mungu alietakasika na  
utukufu wake,na anafanya hali ya

kumtakasia kwake Mwenyezi Mungu  
ibada alietakasika na utukufu,basi  
midhali amekubali kwamba yeye  
Mola,basi kwamba inamlazimu awe  
mwenye kukubali kua yeye ni mwenye  
kuabudiwa,na hakika mwenginewe  
hastahiki chochote katika ibada,**na**  
**dalili juu ya kwamba ibada pekee kwa**  
**Mwenyezi Mungu tamko lake:** (Enyi  
watu!Muabuduni Mola wenu ambaye  
amewaumbeni ninyi na wale  
waliyokuwa kabla yenu;ili  
kuokoka.Mwenyezi Mungu ambaye  
aliyewafanyia ardhi hii kama  
tandiko,na mbingu kama paa na  
akateremsha maji kutoka  
mawinguni,na kwa hayo akatoa  
matunda yawe riziki kwenu,Basi  
msimfanyie Mwenyezi Mungu

washirika,ili hali mnaelewa.)

Albaqarah:22.

Enyi watu:Huuwito kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa watu wote waumini na makafiri,**kwani Mwenyezi Mungu ametaja katika hii sura surat albaqarah vigawanyiko** vya watu watatu:

Kigawanyiko cha kwanza: Waumini ambao wanaamini yasioonekana na wanaamini siku ya mwisho na akawasifu kwamba wao ndio wenye kufaulu katika tamko lake: (**Hao wapo katika uwongofu utokao kwa Mola wao na hao ndio waliofaulu**).

Albaqarah:5.

Kigawanyiko cha pili: Makafiri ambao wamedhihirisha ukafiri na kupinga,**amesema mtukufu:** (Hakika wale waliokufuru ni sawa kwao ukiwaonya au usiwaonye, hawaamini). **Albaqarah:6.**

Kigawanyiko cha tatu: Wanafiki ambao si pamoja na makafiri na si pamoja na waumini (**Wanatangatanga baina ya huku na huko,huku hawako na huko hawako**) Annisaai:143.

Basi wao ni waumini nje lakini wao ni makafiri ndani yake,na wao ni shari kuliko makafiri wenye kudhihirisha ukafiri wao,na kwa hivyo ameteremsha basi kwao sehemu ya aya kumi,wakati ambapo ameteremsha kwa aya za

waumini ni chache,na kwa makafiri  
aya mbili (**kwa ubaya wao**) ama  
wanafiki basi akaanza kuwataja wao  
katika tamko lake: (**Na mionganini mwa  
watu wapo wasemao tumeamini**)  
**Albaqarah:8.** **mpaka katika tamko lake:**  
(**Unakaribia umetaka kunyakua macho  
yao**)**Albaqarah:20.**

Haya yote kwa wanafiki kwa ukubwa  
wa hatari yao na ubaya wa vitendo  
vyao,na pindi alipoeleza hizi aina tatu  
**kasema:** ((**Enyi watu**) huu ni wito kwa  
wote aina waumini,na makafiri,na  
wanafiki,**wamesema**  
**wanazuoni:**Mwanzo wa wito katika  
qur-ani ni huu (**Enyi watu muabuduni  
Mola wenu**) **Albaqarah:21.**

Muabuduni:kwamba takaseni kwake ibada,kwanini? kwamba ye ye Mola wenu,na ibada haitendeki isipokua kwa Mola alietakasika na utukufu,**kisha akataja dalili juu ya hayo nayo tamko lake: (Ambae amekuumbeni nyinyi).**

Na wale ambao kabla yenu nyinyi:katika uma zote (**zilizopita**) ameumba Mwenyezi Mungu alietakasika na utukufu wake kaumba Malaika na majini na wanadamu na viumbe wote.

Ili mupate kuwa wachamungu:**Mukizingatia nyinyi haya,basi huenda hii ikawasababishia uchamungu pindi mukizingatia kwamba ye ye ndie ambae**

amekuumbeni na akaumba ambao  
waliokua kabla yenu,ili mupate  
kumcha yeye alietakasika na utukufu  
wake,ili mupate nyinyi kuogopa  
adhabu yangu na kujikinga na  
moto,kwani kwamba haikukingini  
isipokua ibada kwake yeye Mola wenu  
ambaye amekuumbeni nyinyi na wale  
waliokuwa kabla yenu.

Kisha akaendelea kuwatambulisha  
juu ya Ungu wake na kuabudu  
kwake alietakasika na utukufu wake  
kwa tamko lake: (**Amefanya kwenu  
nyinyi ardhi tandiko**) kwamba  
**busati(Na Mwenyezi Mungu amefanya  
kwenu ardhi tandiko)** Nuh:19.

TNB: Hii ni sehemu ya nne ya kitabu hiki cha

Masomo katika Umuhimu wa Tawheed.

Muhtasari wa kitabu cha (**Al-Usulu AL-Thalathah**)

Kilicho tungwa na Imamu Sheikh Saleh bin Fauzan Al-Fawzan. Bado kinaendelea tufatilie toleo la 5 inshallah.